

# UPATIKANAJI WA ELIMU YA MSINGI

## KWA WATOTO WANAOISHI KATIKA UMASKINI ULIOKITHIRI



***"Elimu hunisaidia kufikia malengo yangu.
Elimu ni ukombozi kwa maisha yangu, familia yangu na kwa jamii yangu".***
*A primary school child, Kinondoni*



# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Muhtasari wa Utafiti | 2 |
| Utangulizi | 4 |
| Mbinu za Utafiii | 6 |
| Matokeo ya Utafiti: Changamoto gani? Ni jitihada gani? | 12 |
| Mapendekezo | 54 |
| Hitimisho | 56 |


© **ATD Dunia Ya Nne Tanzania**

# 1. MUHTASARI WA UTAFITI



### 1.1. Historia

Elimu ya msingi ni moja kati ya misingi mikuu katika maisha. Haki ya elimu ya msingi kwa mtoto siyo suala la mjadala, licha ya upana wa uchumi wa familia ya mtoto, utamaduni au asili ya jamii yake. Hata hivyo, kuhusu watoto ambao wanaishi katika familia ambazo zimezama katika ufukara mkuu uwezekano wa kumaliza mzunguko wa kumaliza elimu ya shule ya msingi unakuwa finyu mno. Utafiti huu shirikishi ulianza tangu Januari 2015 hadi Marchi 2016 katika wilaya ya Kinondoni Dar es Salaam, kuelewa hali sahihi za watoto wanaoishi katika umaskini, kuanza na kumalizia masomo yao katika shule za msingi.

### 1.2. Mbinu

Watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanao ufahamu unaotokana na uzoefu wao adimu wa maisha yao. Mara zote hawatazamwi na waishia kudharauliwa, ufahamu wao wa ndani unaweza kuleta utatuzi muhimu kwa changamoto wanapokaa meza moja na watunga sera. Utafiti ulihamasishwa, kuendelezwa na kusaidiwa na timu iliyohusisha watu wanaoishi katika ufukara uliokithiri na wengine kutoka katika nyanja mbali mbali. Kwa zaidi ya miezi kumi na mitano walihojiwa wazazi arobaini na sita, watoto arobaini walimu ishirini na viongozi wa serikali za mitaa. Njia iliyo bora na sahihi ilitumika kuweza kupata ufahamu mpana kuhusu familia zinazoishi katika ufukara uliokithiri. Katika mbinu hii timu ya utafiti iliweza kufahamu afya ya familia, pato, mahusiano mapana ya kijamii n.k. Yanavyokuwa na athari katika elimu ya msingi ya mtoto na kuibua juhudi zinazofanywa na wadau mbali mbali wanaohusika. Timu ya utafiti ilikuwa bunifu katika jinsi yake ya kukusanya na kuchambua takwimu kuhakikisha kila mtu licha ya asili yake anachangia katika thamani iliyo sawa.
Mbinu hii wakati hali sahihi iliporuhusu ilionesha maoni ya watu wanaoishi katika ufukara uliokithiri kuwa yanaweza kutumiwa katika kutengeneza mabadiliko ya sera ambazo zitaleta msukumo chanya katika jamii zao.

### 1.3. Matokeo

Elimu ya msingi kwa watoto wanaotoka katika familia zenye ufukara uliokithiri kwa mapana imejikita kwa sehemu mkubwa katika muktadha wa familia changanua, na jamii pana, migongano ya ndani na ya nje katika familia na jumuiya, afya na kazi za wazazi usalama na masuala mbalimbali yanayowazunguka na mazingira yote yanayosababisha athari kubwa kwa watoto. Kwa changamoto ambazo zinakuja mara kwa mara na bila kutegemewa, familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri hutafuta ufumbuzi wake kadiri zinavyojitokeza nazo zinaweza kuwa za muda mfupi na zisizoeleweka. Mahusiano kati ya wazazi na walimu yanabadilika, ni ya kulaumiana na kuhukumiana. Watoto wanaogopa baadhi ya walimu wao na hujihisi kutengwa kutokana na asili yao. Yote haya huleta mzingira yenye changamoto kubwa kati ya watoto na walimu.
Hata hivyo nia ya kweli ya kuboresha mahusiano haya ilionyeshwa na wadau. Juhudi zinafanywa, zingine ziko wazi wakati zingine zinahitaji uelewa. Elimu haina umuhimu ambao ni wa lazima kwa watu wanaoishi katika ufukara uliokithiri. Katika changamoto hizi mwalimu anabaki kuwa mtu aliyejitoa kuhakikisha anaelimisha. Watoto kutoka katika familia zilizo katika ufukara uliokithiri huona kwamba elimu ni njia pekee ya kuwatoa katika dhima na tabu zao.

### 1.4. Mapendekezo

Mapendekezo yanaita ushirikiano kati ya washirika mbali mbali wanaofanya kazi katika kujitoa kuhakikisha kwamba mtoto anafanikiwa kuanza na kumaliza elimu yake ya shule ya msingi. Wazazi, walimu, viongozi wa serikali za mitaa na serikali kuu pamoja na jamii katika upana wake washirika wa nje pamoja na watoto wenyewe kila mmoja analo jukumu la kufanya katika utekelezaji wa hili.

# 2. UTANGULIZI



Watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanakabiliwa na changamoto nyingi katika maisha. Tatizo moja, lililojitokeza, inaonekana halina mantiki katika elimu ya msingi ya watoto wao. Katika wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, ambapo utafiti ulifanyika, elimu ya msingi ni bure na watoto wengi wanaishi karibu na maeneo ya shule.

Elimu ya msingi ni moja ya nguzo imara ya maisha. Haki ya mtoto kupata elimu ya msingi ni jambo lisilopingika, bila kujali upana wa historia ya familia, uchumi, utamaduni au jamii. Hata hivyo, kwa watoto wanaoishi katika familia zilizojikita katika umaskini uliokithiri sana, uwezekano wao wa kupata na kumaliza elimu ya shule ya msingi ni mkubwa mno. Wakati mzazi anaona mtoto wake ananyimwa haki muhimu za elimu ya msingi, yeye huona kana kwamba amefungiwa nje ya fursa mbalimbali za kidunia na uwezeshwaji, na maendeleo binafsi ya baadae.

Utafiti huu shirikishi ulifanyika kuanzia Januari 2015 hadi Machi 2016. Mwanzoni mwa utafiti na kwa miaka mingi iliyopita, mazingira ya elimu ya msingi yalikuwa tofauti kabisa na ilivyo leo. Kwa mfano, 87% ya wazazi walitoa taarifa kuwa wamelipa michango ya shule mnamo Juni 2013. (Twaweza walieleza kwa ufupi, No.3 2013). Kuanzishwa kwa mfumo wa elimu bure Januari 2016 kulipokelewa vema na wazazi nchini kote. Mfumo ulishughulikia masuala ya ada na michango ya kila siku katika shule za msingi, masuala ambayo yalikuwa yamegusiwa na wazazi wengi kama itakavyoonekana katika ripoti hii. Hata hivyo, utafiti huu shirikishi unaonekana kwenda mbali zaidi ya suala la michango, ukitoa mapendekezo kwa elimu ya msingi ambayo wadau wote wanaweza kuidhinisha na kujitolea.

Jambo linalokubaliwa sana kuwa umaskini uliokithiri huenda mbali zaidi ya mtu au rasilimali duni za fedha ya familia, likisababisha athari kwa haki za watu kiutamaduni, kisiasa na kijamii, haki zao za uhuru na utu. Umaskini uliokithiri unakuwa ni utaratibu wa kawaida na wa kudumu kwa familia, ukijirudia kizazi baada ya kizazi. Kuvunja mzunguko huu wa umaskini, mchanganyiko wa mambo mbalimbali ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa haki za msingi, na uwezo wa kuchukua majukumu haya ya msingi, lazima ujipange. Elimu ya msingi ni moja kati ya haki za msingi katika maisha ya mtoto, ambazo katika muktadha wa familia changanua, ni kati ya mahitaji yanayotakiwa kwenda sambamba na mpango wa kutokomeza umaskini uliokithiri ili uweze kukamilika. Kunyimwa elimu ya msingi ni ukiukwaji wa heshima ya mtoto.

Upatikanaji si tu suala la uandikishaji. Tanzania nzima kiwango cha jumla cha uandikishaji wa shule ya msingi kilikuwa 96.2% mwaka 2013 (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Elimu kwa Wote (EFA) Ripoti kwa Tanzania bara Novemba 2014). Shule inapaswa kuwa mahali pa kujifunza, kufurahi, kuleta maendeleo na urafiki.

ATD Dunia ya Nne kazi yake kuwawezesha watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kupata haki zao za msingi, kutambulika kama wanachama wenye thamani katika jamii na huleta watu kutoka asili zote kwa pamoja ili kupinga chuki na ubaguzi unaosababishwa na umaskini uliokithiri. Umaskini uliokithiri unaweza kuumiza, kuharibu, kudhalilisha na kutishia maisha. Hata hivyo, wakati hali za haki zinapokuwepo, watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri huweza kugundua na kuvumbua uwezo uliofichika katika miaka mingi ya uzoefu wa maisha. Kuwaleta watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri katika mstari wa mbele katika utafiti huu kutaufanya uwe wa kipekee na shirikishi.

Utafiti huu, ulihamasishwa, ukaendelezwa, ukawezeshwa, ukatekelezwa na kukamilishwa kwa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri na wengine kutoka asili mbalimbali wakiangalia kuelewa na kutoa mapendekezo mbalimbali kuhusu hali gani zitaruhusu watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri kuweza kuanza na kumaliza elimu yao katika shule za msingi.





# 3. MBINU ZA UTAFITI

Katika jamii kwa ujumla thamani ya mtu inatokana na kuwa na ufahamu na nafasi fulani waliokuwa nayo. Watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri mara zote hudharauliwa na kuzuiwa katika masuala muhimu ya kisiasa na majadiliano ya kijamii katika ngazi za kitaifa na hata pia katika familia. Kama mama mmoja alivyosema katika utafiti, *“Umaskini unaondosha heshima ya mtu hata katika familia”.*

Malezi binafsi ya kijamii na kielimu, katika mazingira yoyote, tajiri au maskini, hayawazuii kupata maarifa asilia ya uzoefu wa maisha. Kwa kuwa na ufahamu wa kuchunguza na kujifunza jinsi ya kukubaliana na yale yanayowazunguka, hukusanya maarifa.

Ambapo unatafuta jibu la swali, au tatizo, ni kawaida kumtafuta mtu sahihi wa kujibu swali au kutatua tatizo. Kwa mfano, kama gari imeharibika injini huitwa fundi, pale bomba linapoharibika huitwa fundi bomba, nayo sketi ikitoboka hupelekwa kwa fundi cherehani. Kwa sababu hiyo, wakati unataka kufahamu juhudi na changamoto wanazokutana nazo familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri kuhakikisha watoto wao wanapata haki ya elimu ya msingi, mtu sahihi wa kujibu maswali haya ni mwenye uzoefu wa muda mrefu wa umaskini uliokithiri.

Kuwahusisha wazazi na watoto wanaoishi katika umaskini ulikokithiri, walimu na viongozi wa serikali za mitaa ilikuwa ni mahala ambapo ATD Dunia ya Nne ilifahamu kuwa eneo ambalo utafiti unatakiwa kuanzia. Kuuliza maswali kwa walengwa ni kipengele kimoja cha uelewa, inakupatia taarifa. Hata hivyo, jinsi taarifa inavyofanyiwa uchambuzi ni katika njia ya uwazi na inayoeleweka.

Mwanataaluma wa utafiti ataleta maarifa au uzoefu wake, awe wa kike au wa kiume mwenye uzoefu binafsi wa umaskini au laa, huongeza thamani na nguvu katika utafiti. Vile vile mtu mwenye uzoefu wa moja kwa moja wa umaskini, uzoefu wa kuzaliwa na uzoefu wa maisha ya kila siku, mazingira sahihi yanapotekelezwa kuhakikisha ushiriki wake naye pia huongeza thamani katika utafiti. Swali muhimu la kulizingatia, je, mtu mwenye uzoefu wa moja kwa moja wa umaskini atakuwa sahihi kutambua na kuelewa changamoto zinazowakabili watoto maskini katika kupata elimu ya msingi?

Timu ya utafiti iliundwa mwanzoni mwa mradi. Lengo ni kuwa mhimili wa utafiti, kamati ya muda ambayo itaamua na kuuendesha mradi kusonga mbele. Timu ilikuwa ikiongozwa na ilihusisha jumla ya watu watano amabao wanao uzoefu wa moja kwa moja na umaskini uliokithiri, walimu wawili, mwanafunzi mmoja, kiongozi wa serikalli ya mtaa na wanaharakati wanne wa kujitolea wa ATD Dunia ya Nne. Katika wale wanne wanaoishi katika umaskini uliokithiri, wote aidha wana watoto au wajukuu wanaosoma shule ya msingi. Walimu wawili, mmoja ni mwalimu mkuu wa shule ya msingi ya serikali na mwingine ni mwalimu wa shule ya mtu binafsi. Mwanafunzi alikuwa akisoma chuo cha umma. Waliobakia wanne ni wanaharakati wa kujitolea wa ATD Dunia ya Nne wakitokea katia sehemu tofauti, watatu ni watanzania na mmoja ni mwingereza. Ambao ni wasimamizi wa mradi.

Timu ya utafiti walipata kufahamiana kupitia majadiliano na mikutano iliyokuwa ikifanyika. Hii iliifanya timu ifahamiane vizuri, vipaji, matarajio kwa kiwango cha juu, kufurahia mradi na majukumu tofauti ambayo kila mmoja atakayokuwa nayo. Kwa mfano mwanafunzi alikuwa ametingwa na masomo njia pekee ya kushiriki kwake katika mradi ilikuwa ni siku za mwisho za wiki au siku za mapumziko. Pia ilikuwa hivyo hivyo kwa walimu waliokuwa wakishiriki katika mradi. Watu wawili wanaoishi katika umaskini uliokithiri walijifunza kusoma na kuandika katika kipindi cha miaka miwili au minne kwa mtiririko, ambayo inamaanisha kulihitajika mazingatio sahihi amabayo ushiriki wao unakuwa sawa na wengine katika timu. Kupitia majadiliano haya timu imejifunza kwamba kama watu wanaishi katika umaskini uliokithiri husimamisha shughuli zao na kutekeleza majukumu yao kikamilifu, bila ya kuleta madhara katika familia zao. Wakati wa kuandaa ajenda ya mkutano ilikuwa ni jambo la lazima kuruhusu kila mtu kutoa mchango wake ili kuendeleza utafiti.

Katika mkutano wa kwanza moja ya maswali yaliojadiliwa lilikuwa, je, kuna uhusiano wowote kati yako na shule ya msingi? Hii iliwapa fursa kila mtu katika timu ya utafiti kujieleza namna anavyojihusisha na masuala ya elimu ya msingi akiwa kama mzazi, mwalimu mkuu, mwanafunzi n.k. Timu ya utafiti iliweza kujua kuwa mmoja kati yao alikuwa na jukumu la watoto wanane ambao walikuwa katika shule ya awali au sekondari, na mwanafunzi alijihusisha kuendeleza mradi kwa wasichana ambao waliacha shule ya msingi.

Kisha timu ya utafiti ilifikiria mbinu ya kutumia katika uendeshaji utafiti, mafunzo gani yanatakiwa kwa watafiti? Watu wangapi wanatakiwa kufanya utafiti? Namna gani taarifa zitachukuliwa, kwa kuandikwa, kinasa sauti au video? Siku na muda gani mzuri wa kufanya mahojiano na watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri? Mahala gani pa kufanyia mahojiano, nyumbani kwao, ofisi ya ATD au sehemu tulivu. Mambo yote haya yalikuwa ni muhimu kuzungumziwa na timu ya utafiti ili kuweza kumsaidia mtu atakaye hojiwa kuwa huru kuzungumza na kujiamini wakati anapohojiwa.

Kulikuwa na baadhi ya vigezo kwa watu waliohojiwa, kwa mfano ni lazima awe na watoto wanaokwenda shule, aidha awe mzazi wao, bibi au mlezi na awe katika sehemu iliokusudiwa. Kwa Dar es Salaam kuna maeneo yaliobainishwa, Tandale na Tegeta.

Iliamuliwa kuwahoji wazazi arobaini na sita wanaoishi katika umaskini uliokithiri, watoto arobaini wanaotokea katika familia maskini na walimu ishirini au viongozi wa serikali za mitaa waliobainishwa.

Idada isiyoyakawaida ya wazazi arobaini na sita watakao hojiwa ilitengenezwa kama sehemu ya mbinu ya utafiti. Familia sita zilihojiwa kwa kipindi cha mfululizo wa kila wiki kwa mada tofauti ambazo zilihusisha mambo mengi juu ya maisha yao. Mada zilikuwa, Binafsi, Kipato, Afya, Familia na Marafiki, Makazi na Jamii na Shule. Kutumia njia hii, ambayo ilitengenezwa kutokana na kijitabu *(Sustainable Liverhoods Handbook, Oxfarm 2009)*. Utafiti ulijaribu kuingia kwa kina zaidi iwezekanavyo kwa familia hizi sita kujibu maswali ya utafiti.

Taarifa zilizopatikana katika familia sita zilizohojiwa imeongeza na kuhalalisha utafiti uliofanyika kwa kina katika familia sita. Kuwahoji watoto, walimu na viongozi wa serikali za mitaa ili kutafuta taarifa zaidi na kuzifahamu. Hii italeta mambo mapya kwa ajili ya uchambuzi na kuifanya timu ya utafiti kuongeza mapendekezo kutoka kila pembe.

Kadiri timu ya utafiti ilipoingia kwa kina zaidi katika kuuelewa mradi, walikutana na changamoto zilizowazunguka. Kwa mfano, ilisisitizwa kwa kila mahala utafiti ulipokuwa ukifanyika kulihitajika kibali, aidha katika jamii ya Tandale au shuleni. Barua ya ruksa husika ilipatikana kutoka serikali za mitaa, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Elimu ya Msingi Kinondoni.

Timu ya utafiti ilishughulikia suala la usiri. Umuhimu wa usiri ulijadiliwa na maeneo gani ya kazi yalitakiwa kubaki katika usiri na kwa nini. Watu wawili waliteuliwa na timu ya utafiti na kutengeneza sera ambayo ilisomwa na wanatimu wote. Walikubaliana na kutia sahihi. Kila mtu alitenda ipasavyo katika utafiti na kuheshimu sera za utunzaji siri. Timu ya utafiti iliweka utaratibu wa kufuata endapo wakiambiwa au kutokea kitu hawakikufurahi wakati wa utafiti.

Timu ya utafiti walitambua kwamba ilikuwa ni muhimu kwa watu watakaohojiwa kufahamu watafiti ni wakina nani na kusudio la ujio wao. Utambulisho wa mradi uliwasaidia watu kuelewa kuwa watafiti hawapo pale kwa kutatua matatizo yao. Ilikubalika kwa kila mtafiti kuwa na kitambulisho chenye picha yake amabacho watakionyesha wakati wa kujitambulisha. Wakati wa kufanya kazi katika makundi madogo ya watu wawili au watatu kufanya mahojiano, walibeba nakala za vibali zilizotolewa na mamlaka husika.

Kwa kila mahojiano, kila mhojiwa alitembelewa kwanza na kuelezewa kuhusu mradi kabla ya mahojiano kufanyika. Hii iliwafanya watu kuwa huru kuamua na kuwa tayari kuendelea na maandalizi ili kuweza kuwa huru siku ya maandalizi. Hivi vipengele vidogo vidogo viligharimu muda mwingi lakini vilikuwa hatua muhimu kama ilivyokuwa imekubalika katika timu ya utafiti.

Kuendelea na kukubaliana juu ya maswali kwa ajili ya mahojiano ilikuwa kazi nyingine ya Timu ya Utafiti. Kama ilivyoeleza, mada sita kuimarisha utafiti, mtiririko wa maswali ulipangiliwa, sio wakuchosha, wakati huo huo ukiweza kuchunguza kwa kina na kupata taarifa zinazohitajika.

Kamati ndogo iliundwa kufanya kazi ya kuunda maswali, ilikuwa na watu wawili walio na uzoefu wa umaskini, wanaharakati wawili wa kujitolea wa ATD na mwanafunzi. Kwa muda wa zaidi ya wiki mbili, walikutana katika sehemu tofauti kujadiliana, kukubaliana na kuandika orodha ya maswali kwa ajili ya familia sita, familia arobaini, watoto arobaini na walimu ishirini na viongozi wa serikali za mitaa. Orodha ya maswali haya hatimaye yalithibitishwa na timu ya utafiti.

Hatua iliyofuata katika kuboresha utafiti ilikuwa ni mafunzo namna ya kuwahoji watu. Siku ilitumika kwa kuelezea mradi, namna watafiti watakavyoweza kujitambulisha na kuyaelewa maswali. Mafunzo yaliotolewa ni namna ya kutumia kifaa cha kunasa sauti na kamera. Kisha timu ilifanya mazoezi ya mbinu za kufanya mahojiano. Walifahamu namna ya kumshawishi mtu anayehojiwa kujibu maswali kwa kina zaidi, namna ya kumwongoza mtu kujibu swali aliloulizwa, kitu cha kufanya iwapo mahojiano yataingiliwa na mtu asiyehusika kwa mfano mgeni anayekuwa amefika nyumbani, n.k.

Mtu mwenye uzoefu wa kuishi katika umaskini alielezea kwanini ilikuwa muhimu kuhojiwa na mtu mwenye hali kama yake. Alisema:

- *Mtu anaenihoji anatakiwa kufahamu hali niliyo nayo. Atakuwa mwangalifu aina gani ya maswali anapaswa kuniuliza. Atajua maswali gani aniulize na yapi asiniulize ili isiwe tabu kwangu.*

- *Iwapo mtu anayenihoji atanifanya nijiamini, kuonyesha kuwa hali zetu zote ni sawa, atanihamasisha kumuonyesha zaidi kuhusu maisha yangu na kile anachohitaji kukijua.*

- *Nitakuwa na uhakika kwamba kile nitakachomwambia kitawekwa na itakuwa ni siri.*

Njia zingine za utafiti za kijadi kwa kuthibitisha takwimu nazo pia ziliingizwa katika mbinu. Hizi ni pamoja na kupanga kabla siku ya mahojiano na muda ili kuruhusu mabadiliko, kutumia njia rafiki wakati wa mahojiano ili kutengeneza mwelekeo wa maswali hivyo kuweza kurejea katika maandishi yaliyotayarishwa pamoja na watoa taarifa.

Mahojiano na wazazi yalianza mwezi wa nne 2015, yakafuata ya walimu, viongozi wa serikali za mitaa na hatimaye watoto na yalimalizika mwezi wa Desemba 2015. Katika kipindi chote hiki kila mahojiano yaliandikwa kwa uangalifu na kuangaliwa tena kupitia kinasa sauti.

Desemba mwaka 2015 kazi ya kuchambua taarifa ilianza baada ya kufanya mahojiano zaidi ya 100, na mamia ya kurasa za takwimu, rekodi na video. Mchanganyiko wa watu katika timu ya utafiti, ulikuwa na maana kwamba ubunifu ulikuwa unahitajika kutafuta namna ya kufanya kazi kwa pamoja kwa amani na kuwa na mipaka ya kuheshimiana na kuthamini mchango wa kila mmoja.

Lengo la uchambuzi lilikuwa kutafuta changamoto na juhudi ambazo wazazi, watoto, walimu na viongozi wa serikali za mitaa hufanya kuhakikisha kwamba watoto wanaweza kuanza na kumaliza elimu yao ya shule ya msingi. Katika eneo pana la maisha ya familia timu iliona mahusiano katika afya, makazi, kipato n.k. na jinsi maeneo haya tofauti yalivyo na athari katika elimu ya mtoto wa shule ya msingi.

Ilikuwa changamoto kubwa, haikuwezekana kabisa, kumpatia kila mtu aliyekuwa katika timu ya utafiti kila mahojiano tulioyafanya kusoma. Timu iligawanyika katika makundi madogo kuchambua mada za utafiti (Binafsi, Kipato, Afya, Familia na Marafiki, Makazi na Jamii, Shule) na mahojiano ya walimu, viongozi wa serikali za mitaa na watoto. Baadhi ya mahojiano yalifanyika kwa kutumia kinasa sauti na kuchukua video. Hii iliwapa fursa kwa wale walikuwa hawajui kusoma vizuri katika makundi madogo kuchambua bila ya kuwa na mlolongo mrefu wa kusoma. Muda mwingine wa kufanya kazi katika makundi madogo kusoma kwa sauti, kwa taratibu kurasa hadi kurasa ili kumwezesha kila mmoja kutoa maoni yake kwa kile alichokipata. Timu ilifanya kazi katika makundi madogo hadi kupata mapendekezo ya pamoja. Ripoti ya mwisho ya utafiti iliandikwa mwezi Aprili 2016.

# 4. Matokeo ya Utafiti: Changamoto gani? Ni jitihada gani?

Utafiti uliambatana na mada sita tofauti kufuatanana maisha ya watu: binafsi; familia na marafiki; nyumba na jamii; fedha; afya na shule Taarifa zilizokusanywa zilitolewa kwa pamoja na kuchambuliwa kutokana na kila mada.
Matokeo ya utafiti yaliruhusu kundi la utafiti kufanya hitimisho na mapendekezo kwa wazazi, walimu, serikali za mitaa na kitaifa, na wadau wengine wa elimu.




CnM

### 4.1. Binafsi

Familia sita ambazo utafiti ulilenga kuingia kiundani waliulizwa maswali kuhusu wao wenyewe binafsi. Baadhi ya maswali hayo yalikuwa ya binafsi sana, kama vile kabila lao, ambapo wametokea idadi ya watoto na kama wao wana simu za mkononi. Maswali mengine yalikuwa wazi zaidi, kama vile wanajivunia nini na kitu gani wanapenda.

Kuhusu cha kujivunia, wazazi wote walisema wanajivunia watoto wao wanaosoma. Wote waliona watoto wao kama tumaini la familia kuwa na maisha bora ya baadaye, na kuwa na uwezekano wa kutafuta kazi. Wazazi wanaamini maisha yao yatakuwa salama kupitia watoto wao. Kama maisha ya watoto wao yatakuwa salama na yao pia yatakuwa salama.

Wazazi wengi walisema hawakuwa na kitu cha kujivunia kuhusu wao wenyewe. Wana mawazo mafupi juu ya maisha. Mama mmoja alisema,

> *"Tatizo ni hatuna mtazamo wa muda mrefu, hufikiri ya sasa na si ya baadaye. Hatufikirii vitu vitakavyo kuwa wakati tutapoamka siku inayofuata, au leo niko hai lakini vitu vinabadilika. Hatujui".*

Kwa mama huyu kutokuwa na mipango ya baadaye kulimwacha yeye na familia yake katika hali ya kutokuwa na uhakika; akiwa hajui kitakachotokea kesho, kamwe bila udhibiti wa maisha yake.

Baba mmoja alisema alikuwa akijivunia kumiliki ardhi yenye vyumba viwill, aliendelea kusema, *"Ninajivunia na maisha ambayo Mungu ametupatia".* Kumshukuru Mungu lilikuwa ni jambo muhimu sana kwa familia zote zilizohojiwa. Baba mmoja aliendelea kusema atajivunia siku moja kuwa kiongozi katika jamii yake. Alisema,

> *"Natamani kungekuwa na uwezekano siku moja kuwa kiongozi. Wakati naona watu wananyimwa haki zao natamani ningekuwa na elimu ya kutosha ingenifanya kuwa kiongozi imara mwenye kuweza kusimamia haki zao kwa sababu naona watu wanaonewa, inaniuma sana".*

Kuhusu maisha ya baadaye mama maskini sana alisema yeye ana ndoto siku moja kuwa mwigizaji. Alisema kuhusu kipaji chake chakufanya watu kucheka katika jamii yake na kwamba yeye alikuwa anajulikana kama *"mchekeshaji"*.

Asilimia arobaini ya watu waliohojiwa walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Wengi kati yao hawakumaliza elimu ya msingi, baadhi hawakwenda shule kabisa. Wazazi wengi walizaliwa na kukulia vijijini nje ya Dar es Salaam. Wengi

wao, hufanya kazi za nyumbani, kulima, kuangalia wanyama ndio yalikuwa maisha yao ya kila siku na ndiyo sababu iliowafanya kutohudhuria shule.

Kila mzazi aliyehojiwa aliulizwa kama aliwahi kusafiri ndani ya nchi au nje. Wote walisema walisha waihi kusafiri ndani ya Tanzania kutoka au kurudi kijijini kwao kwa nyakati tofauti. Hakuna aliyesafiri nje ya Tanzania.

Umiliki wa simu za mkononi, baba wote waliohojiwa wanamiliki simu, lakini wamama wengi hawamiliki. Baadhi ya wamama walikuwa wanamiliki simu siku za nyuma, au ikitokea dharura huazima simu kutoka kwa jirani. Mama mmoja alisema kwamba kumiliki simu alikuwa inasababisha kutoelewana na mume wake kwa sababu hakuwa na imani naye na alitaka daima kufuatilia na kuangalia nani alikuwa akimpigia.

Moja ya maswali ya mahojiano yalikuwa kama wazazi wana marafiki. Asilimia sitini na tano 65% walisema ndio na 35% thelathini na tano hapana.

## 4.2. Familia na marafiki

### 4.2.1. Kupambana na matatizo

Familia zinakabiliwa na migogoro na kutafuta ufumbuzi ni kitu ambacho wazazi wote walikiongelea kwenye majadiliano kuhusu hilo. Migogoro na kutokubaliana kati ya wazazi wanaweza kumwaathiri mtoto kielimu.

Wakati familia haina amani daima huwa katika hofu na migogoro, inaweza kupelekea watoto, kukimbia familia na kuishi katika mitaa. Mzazi mmoja alisema,

*"Kama wazazi wapo kwenye migogoro, wakati mtoto akiwa shule huwaza mara kwa mara kuhusu nini kinaendelea nyumbani, hii inafanya mtoto kusikitika na hatoweza kujifunza".*

Wazazi wana wasiwasi nini kinaweza kutokea kama watu hawawezi kupatanisha tofauti zao. Mama mmoja alisema, *"Kama baba ataoa mke mwingine, wakati mtoto anakwenda shule na walimu kumuuliza mtoto kuleta michango mtoto huwa na wasiwasi kwenda nyumbani na kumwambia mama wa kufikia".* Kutengana kwa wazazi kunaweza kuleta mashaka kwa watoto wapi wataenda kuishi. Hii inaweza kuwa sababu nyingine, kuwafanya wazazi wapi wanaweza kuwapeleka watoto wao shule. Wakati mwingine mzazi anataka kuishi na mtoto kutokana na sababu tofauti, lakini kama hakuna shule karibu elimu ya mtoto inaweza kuathirika.

Baadhi ya watoto wanaishi na wazazi wasiowazaa. Hii inaweza kuwa na maana kwamba baadhi ya watoto *“wanapendwa”* zaidi ya wengine. Kwa mfano, kama baba katika familia ni baba wa watoto wadogo, inatokea katika baadhi ya familia hukataa kuwasaidia watoto wakubwa, ambao sio wa kwake. Katika familia nyingi wazazi huonyesha upendo sawa kwa watoto, kuwajali na kutoa msaada kwa wote.

Pesa inaweza kuleta mvutano katika maisha ya familia, kati ya mume na mke, kati ya wazazi na watoto. Mama mmoja alisema yeye hampendi mumewe, kwani huwa juu na kudhibiti kila kitu. Mume wake hamruhusu kufanya kazi, hivyo yeye husimamia kila kitu nyumbani. Kwa maana kila kitu akitaka kununua lazima amuulize mume wake, hata watoto wanamuomba Tzs 50 kununua pipi, hana budi kumuuliza mumewe. Alisema kumuomba mumewe mara kwa mara ni kama kumfedhehesha.

Viongozi wa serikali za mitaa waliohojiwa pia walisisitiza umuhimu wa umoja wa familia kukubaliana na wazazi kwamba kutokuelewana kunaweza kuwavuruga watoto katika masomo yao. Pia walitengeza kipengele kwamba tatizo linaposhindikana kutatulika na wazazi wakatengana, mama hukabiliana na changamoto za kulea na kuwasomesha watoto bila uongozi na maelekezi ya baba.

Mzazi mmoja alielezea matatizo haya kwa muhtasari, alisema,

“*Udhaifu wa mapatano ya familia hufanya watoto kuishi katika hali ya hatari".*

### 4.2.2. Kuweka juhudi na kutafuta ufumbuzi

Ufumbuzi wa matatizo, kwanza yanaweza kupatikana katika familia, lakini pia kwa upana zaidi wazazi kushirikiana matatizo yao na majirani zao na kuhamasishana kila mmoja. Mama mmoja alisema hupiga simu nyumbani kwa familia yake kijijini na kupeana habari. Baba mmoja alipohojiwa alieleza kuwa mtoto alikwenda kuishi na shangazi yake ambako kakulia na kupelekwa shule. Sisi tuligundua kwamba miongoni mwa baadhi ya familia tulozozihoji walikuwa wanalea watoto wa ndugu zao. Si tu wazazi lakini familia changanua kwa pamoja wote hushirikiana katika kulea watoto na elimu yao ya shule za msingi.

Katika mahojiano na mama mmoja alionyesha kwamba mtoto akienda shule kila siku ilimtia moyo mzazi na hivyo kupambana kupata fedha kila siku, na kwamba wakati mtoto anapoona mama yake anajitahidi kila siku ili kupata pesa pia ilikuwa motisha kwa mtoto kwenda shule. Mzunguko huu wa kutiana moyo kati ya mzazi na mtoto ni muhimu katika familia maskini ambapo jitihada nyingine mara nyingi hazitambuliwi.

#### 4.2.3. Shughuli za ziada

Kila familia ina majukumu. Hii ni pamoja na watoto kupewa kazi za nyumbani wakati anaporudi nyumbani au kabla ya kwenda shule. Hii huchukuliwa ni njia muhimu kwa mtoto kuwa sehemu ya familia na kuwasaidia kufahamu shughuli muhimu za nyumbani. Wazazi walisema wakati mtoto anaporudi kutoka shule na kupewa kazi za nyumbani kwa muda mfupi kabla ya kufanya kazi alizopewa shule, inawasaidia kuchangamsha akili zao. babu mmoja alijivunia majukumu anayompa mjukuu wake, *"Najivunia masomo ya wajukuu wangu. Sijui kusoma na kuandika, ninapopata barua huwaita wajukuu zangu ambao hunisomea vizuri, neno kwa neno. Hii ni bora kuliko kumpelekea jirani yako kwani anaweza kuzidisha au kupunguza maneno katika barua. Hii inanifanya nijivunie wajukuu wangu".*

Watoto waliohojiwa walizungumza kuhusu shughuli wanazofanya nyumbani. Wachache tu huwa hawafanyi, hata hivyo wengi walihusika katika baadhi ya kazi za nyumbani: kusafisha nyumba; kuosha nguo; kupika. Hii ni kwa wote wasichana na wavulana. majukumu mengine yalikuwa ni kuwasaidia wazazi wao kufanya biashara ili kuongeza kipato. Mtoto mmoja aliwasaidia wazazi wake kazi ya duka baada ya shule, na endapo baadhi ya siku wazazi wake wakiwa wameenda mahali hufanya kazi hizo na kushindwa kwenda shuleni. Kwa watoto waliohojiwa, wengi husaidia shughuli ndogo jioni. Ilisemekana wengi walikuwa wakiuza vitu kama karanga au ubuyu, mtoto mmoja husaidia kutunza wanyama. Mtoto mmoja huuza CD mbele ya nyumba yao, mtoto mwingine huuza maji ya chupa. watoto kadhaa walisema mwishoni mwa wiki huwasaidia wazazi katika biashara zao ndogo ndogo. Mtoto mmoja alimjibu mtu aliyekuwa anamhoji kwamba,

> *"Wakati wa kurudi nyumbani sina muda wa kusoma, huenda katika soko na kuokota mahindi yaliomwagika chini na kuuza kwa kilo na pesa hutumia shule au humpatia mama yangu".*

Baadhi yawazazi walizungumzia jinsi ya wanavyo jisikia faraja kuona watoto wao wanaporudi nyumbani kutoka shule na kuungana nao katika shughuli kama vile kuvunja mawe ili kupata pesa. Walisema hiki kidogo wanachokipata kinawezekana kikawa chanzo kusaidia kwenda shule. Mama mmoja alisema,

> *"Jumamosi humtuma mwanangu kuzunguka mitaani kutafuta mawe ili tuweze kujazaa ndoo na kuweza kuuza".* (Ndoo moja ya kokoto inaweza kuuzwa shilingi 300)

Wazazi walitoa mifano ya kile wanachopenda kufanya: kutumia muda na watoto wao kukaa na kusikiliza hadithi zao kile kilichotokea katika siku hiyo; kujifunza kusoma na

kuandika na kuwa na mafunzo ya ujasiriamali; kujifunza ujuzi wa kisanii kama kufuma shuka; kuwa na upatikanaji wa internet, habari hadithi na kuelewa teknolojia mpya. Familia chache zina luninga na wanaangalia nyumbani. Kwa familia ambao wana TV, ilichukuliwa kuwa na matokeo chanya na hasi juu ya elimu ya watoto. Wazazi walisema baadhi ya vipindi vya TV vinaweza kuwa elimu na kujifunza kwa mtoto. Hata hivyo, wazazi wengi walisema Tv si kitu kizuri kwa watoto. Kwa wengine inakuwa ni usumbufu wakati wa kusoma, au watoto watatumia muda mwingi kuongea na rafiki zao shuleni kuhusu kitu ambacho walikiona kwenye TV jana usiku badala ya kusoma. Baba mmoja alizungumza kwa msisitizo juu ya hili, *"TV ina athari kubwa. Mtoto anaweza kuulizwa swali shuleni na kushindwa kujua jibu lakini anaweza kukumbuka kile alichokiona kwenye TV ".*

### 4.2.4. Matarajio ya baadaye

Wazazi walikuwa na mipango mbalimbali kwa ajili ya wao wenyewe, kwa watoto wao hapo baadae. Baadhi ya wazazi walizungumzia ndoto zao za kuanzisha biashara ndogo ndogo ili kuwapatia mahitaji muhimu familia zao. Walipoulizwa kama kuhudhuria shule ni kuwasaidia kuwaandaa watoto kwa ajili ya baadaye, na ni shughuli au kazi gani wazazi wangependa wafanye, wazazi wote walisema kuwa elimu ya msingi ilikuwa ni kivuko muhimu katika maendeleo ya watoto wao ambacho kinaweza kusababisha fursa nyingine. Wengi hawakuwa na mawazo maalum ya aina ya kazi ambazo wangependa kuona watoto wao kufanya. Wote walikuwa wa kweli kuongelea taaluma kulingana na kiwango cha elimu ambacho mtoto anaweza kufikia, na kitu cha kulinganishwa na kiwango chao cha mahitaji ya maisha na jamii, Mama mmoja alitoa mfano wa mtoto wake kuwa fundi seremala. Ilikuwa ni muhimu kwa wazazi kwamba watoto wanapaswa kuwa na uhuru wa kuchagua wenyewe. Kumaliza shule ya msingi huongeza fursa kwao kuweza kuchagua na hivyo kuwepo na uwezekano wa kupata uhuru wao.

Alipoulizwa ni nini wangependa kufanya katika siku zijazo, watoto walikuwa na matarajio mengi. Aina ya kazi ambazo wangependa kufanya ni pamoja na kuwa: daktari, mwalimu, mwanajeshi, msanii, karani wa benki, nahodha wa meli, mkulima, mhasibu, mbunge, mfanyabiashara, afisa wa polisi, dereva, mhandisi; na rais. Watoto wote walikuwa na ndoto za kitaaluma, hakuna waliosema hawajui wangependa kuwa nani. Baadhi ya watoto walikuwa na majibu yao maalum.

> *"Nataka kuwa daktari, kutibu watu katika jamii yangu kwa njia nzuri", "Nataka kuwa mwalimu ili niweze kufundisha watoto ambao hawezi kufundishwa"* na *"Nataka kuwa mwanajeshi ili niweze kuzuia mambo*

*mabaya yasifike nchini mwangu kinyume cha sheria, kama madawa ya kulevya, silaha haramu, na watu wanaofanya hivyo kwa sababu ya rushwa".*

### 4.3. Makazi na jamii

#### 4.3.1. Makazi

Kuwa na nyumba ni muhimu kwa maisha imara. Kwa watu maskini, wengi hupambana ili kufikia hatua hii muhimu. Kuishi katika nyumba ya kukodi kunaweza kuleta ukosefu wa usalama, fujo na kuyumba kwa asili ya maisha ya watu, hii humaanisha kwamba ni vigumu kuipata fedha kwa ajili ya kodi kuzidi kipato chao kidogo.

Watu walitoa mifano mbalimbali kuhusu jinsi wao wenyewe wanavyojiandaa kulipa kodi. Utafiti uligundua kwamba watu wengi hushiriki katika miradi midogo ya kuweka akiba wakishirikiana na makundi ya majirani na marafiki, ambapo wao hulipa kiasi kidogo cha fedha kila siku au kila wiki, na baada ya kipindi cha muda fulani hupokea kiasi kikubwa cha fedha sawasawa na kile walichoweka.

Watu walizungumzia umuhimu wa kujiandaa wenyewe, kama vile kuwasiliana na mwenye nyumba, ambao inaweza kuwa katika makubaliano mazuri, au kwa njia mbaya na ya kufedhehesha. Mama mmoja alisema, *“kama angejua majuma kadhaa kabla kuwa itakuwa vigumu kulipa kodi inayofuata, angeweza kuwasiliana na mwenye nyumba na kuomba aongezewe muda”.* Kutoa taarifa mapema kwa mwenye nyumba ilikuwa muhimu na mara nyingi majadiliano na makubaliano hupatikana. Wazazi wengine walizungumzia mazoea tofauti kabisa na ya kudhalilisha. Baadhi ya familia waliambiwa *"waombe"* au *"waibe"* ili walipie kodi kwa wenye nyumba waliokuwa wagumu kuelewa. Mama mmoja alisimulia yale aliyopitia, *"kumsihi"* mwenye nyumba kwa *"kumpigia magoti"* ili amsubiri afanye kazi na kupata pesa za kumlipa.

Wazazi waliulizwa kuhusu wasiwasi walio nao, mojawapo ikiwa ni kutafuta fedha kwa ajili ya kodi. Haya mashaka pia huathiri watoto kwa kiasi kikubwa. Familia kadhaa zilisema kuwa watoto hushuhudia wazazi wao wakipambana katika kupata kodi, wanaona malumbano yao na wenye nyumba, na watoto huweka yote haya katika akili zao. Mama mmoja alisema *"Kuwa mtoto wake huamka usiku na kumuuliza. Tutafanyaje na hatuna pesa ya kulipia kodi?"*. Yule mama akasema, *"Mwanangu atayaweka yote haya akilini akiwa shuleni, bila kujua wakati atakaporudi nyumbani kama familia yake itakuwa na mahali pa kulala usiku huo".*

Utafiti ulionyesha kuwa idadi kubwa ya wazazi wanaoishi katika eneo la Tandale wamekodi nyumba zao, wakati baadhi ya watu nje kidogo ya mji wa Dar es Salaam

walikuwa wamiliki nyumba. Umiliki wa nyumba ulitoa kiasi kikubwa zaidi cha utulivu kwa familia hizo, ingawa si kutoa utulivu kamili.

Habari za kujipatia kiwanja, mama mmoja alizungumzia watu maskini katika baadhi ya maeneo kama kuwa *"Wavamizi"*, akimaanisha wangeweza kupata kipande kidogo cha ardhi na kujenga makazi. Haya makazi madogo madogo yasiyopangwa yanaweza kudumu kwa muda mfupi au kudumu sana kwa miaka kadhaa. Wakati mwingine makazi haya yalikuwa ni mwanzo wa vijiji na miji mipya, kama inavyoonekana katika eneo la zamani la machimbo ya mawe, Kunduchi. Kwa sasa panatambuliwa kama mji mpya. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo makazi haya yapo katika hatari ya kuharibiwa na serikali, mmomonyoko wa udongo, hali mbaya ya hewa, nk. Migogoro ya ardhi ni ya kawaida, na wakati mwingine wamiliki au serikali hujaribu kuidai hiyo ardhi baada ya miaka kadhaa.

Watu wanaoishi katika umaskini ulikithiri wanaweza kuwa katika hatari ya kupoteza makazi yao kwa wavamizi wenye nguvu. Katika baadhi ya matukio, wakati thamani ya ardhi ikiongezeka, walowezi wapya hujaribu kuiba ardhi kutoka kwa walowezi wa kwanza, ambao mara nyingi huwa ni watu maskini. Wavamizi wenye mabavu hufanya hivyo kwa kununua viwanja na kuongeza ukubwa wa viwanja vyao kuelekea kwenye maeneo ya majirani maskini. Wakati mwingine watu maskini hutishwa na kufukuzwa kutoka kwenye makazi yao. Kwa familia zinazoishi katika nyumba zao wenyewe, ni muhimu wao kufanya ufuatiliaji juu na kupata nyaraka sahihi ili kuhakikisha umiliki wa maeneo yao yamehifadhiwa katika kumbukumbu za ofisi za serikali za mitaa.

Kupitia utafiti ilibainika kuwa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanaishi katika tishio la kubomolewa makazi yao. Wakati mwingine hii inaweza kuwa sio sahihi, hata hivyo inaweza pia kuwa kweli na watu wakaondoka bila ya kuwa na chochote, mali zao zikiwa zimeachwa njiani.

Hata wakati kiwanja kinapokuwa kinamilikiwa na mtu maskini, pamoja na wao kuwa na nyaraka zenye kuthibitisha haki yao ya umiliki, huweza kuleta matatizo. Mama mmoja alizungumza kuhusu tatizo la urithi, ambalo huweza kusababisha malumbano na mvutano kati ya ndugu wakati ambapo kiwanja hugawanywa au kuuzwa na fedha kutogawanywa kulingana na makubaliano kati ya ndugu.

Kupitia utafiti tulijifunza kwamba watu maskini ni wabunifu sana. Watu kadhaa ambao wana mashamba yao wenyewe wamejenga nyumba za jadi za matope na kuonyesha kwamba wanao ujuzi wa kujenga nyumba za aina hiyo. Wakati mwingine ilikuwa muhimu kuchukua mikopo ya kununua mbao na mabati kwa ajili ya paa na baada ya muda kuweza kujenga nyumba ambayo wanaweza kuishi bila kulipa kodi. Tumeweza pia kujifunza kupitia familia moja

inayoishi nje ya Dar es Salaam kwamba ilikuwa inawezekana kupata mikopo midogo kutoka benki kununua vifaa vya kujengea nyumba. Hii iliwezekana kwa sababu benki ilikubali kiwanja kama dhamana katika ulipaji wa mkopo. Kuwa na mkopo wa benki ni kipindi cha kusumbuka hadi mkopo unapokuwa umelipwa kwa ufahamu kwamba kiwanja kinaweza kuchukuliwa na benki. Hata hivyo, mara mkopo ulipolipwa na nyumba kujengwa ilileta utulivu mkubwa kwa familia hakika hii ilikuwa uzoefu chanya.

Kutokuwa na uwezo wa kupata fedha kwa ajili ya kodi ya kila mwezi ni moja ya hofu kubwa kwa familia maskini. Mama mmoja alisema ilifanya maisha rahisi kidogo kwake kupeleka watoto wake shule. Mzazi mwingine ambaye anamiliki nyumba yake mwenyewe alisema kuwa ingawa maisha yalikuwa magumu, ilikuwa ni bora zaidi kulikowakati ambapo familia ilikuwa na chumba cha kupanga.

### 4.3.2. Jamii

Wazazi waliohojiwa walikuwa wazi sana kuzungumzia kuhusu ushiriki wao katika jamii yao, kile wanachokiona kuwa msimamo wao ndani ya jamii, nini changamoto zinazowakabili, na kwa njia gani wanahisi wao ni sehemu ya kujenga jamii zao.

Wengi wao walisema ndani ya jamii zao walikuwa na urafiki kwa kila mmoja, kusalimiana wanapopishana, kushiriki katika matukio kama vile mazishi na kuhudhuria mikutano. Mama huyu alisema,

> *"Kama majirani tunaishi pamoja vizuri, tukiona mtoto haendi shule, tunauliza kwa nini na tunampeleka mtoto kwa mama yake. Tumeungana katika kuhakikisha kuwa watoto katika jamii yetu wanakwenda shule. Hatutaki mtoto awe anazurura tu na kucheza".*

Baba mmoja alielezea kuhusu ugunduzi wake wa eneo jipya ambako alikwenda kuishi, pale jamii ilijipanga na walikuwa na msisitizo kuhusu umuhimu wa elimu. Baada ya shule kila siku, watoto wa jamii ile hujikusanya katika mahali pa mkutano kukaa na kufanya mazoezi ya nyumbani pamoja. Husaidiana na kuhamasishana kila mmoja kujifunza.

Wazazi walisema kwamba, kuwaona watoto wao wakijiheshimu vizuri ni muhimu sana. Ina maana wao wataonekana vizuri ndani ya jamii kwa wazazi wengine na watoto, na mtoto mwenye tabia nzuri hataileteа aibu familia yake. Pia ilikuwa muhimu kwa wazazi kuheshimiwa na watoto wao, na hili hutokana na tabia nzuri. Kusalimiwa asubuhi, wakati watoto wanaporudi nyumbani kutoka shule,

na kushiriki katika kazi za familia wanapoombwa ni dalili ya tabia nzuri ambazo zinahamasishwa na wazazi.

Baadhi ya familia walisema kuwa wanao uhusiano mzuri na majirani zao kama wataunganishwa kupitia makundi ya kidini. Familia zote zilisema kuwa ni muhimu sana kwao kuishi kwa amani, lakini maseng'enyo na kashfa mara nyingi zilikuwa ni sababu ya migogoro.

### 4.3.3. Changamoto na hofu ya jamii

Wasiwasi mkubwa wa wazazi ni kuhusu idadi ya watoto wanaozunguka mitaani na kutokwenda shule, na athari zinazochochea muundo huu mbovu kwa watoto, hususan tabia mbaya wanazoweza kujifunza miongoni mwao. Baba mmoja alizungumzia kuhusu hali tete inayotokea katika jamii kuanzia kwa watoto. Alisema kwamba watoto wanaweza kucheza wakati fulani na baadae kugombana. Wazazi ni huwalinda sana watoto wao na mara nyingi huwakaripia watoto wengine wanapowaona wanagombana, jambo ambalo linaweza kusababisha migongano kati ya wazazi wa wale watoto. Wakati mwingine kutoelewana kati ya wazazi ni hali inayoweza kudumu kwa muda mrefu, na kuleta uhasama mkubwa ndani ya jamii, wakati watoto wamerejea tena kucheza pamoja.

Kukosekana kwa ushirikiano kati ya wazazi katika jamii kunaweza kuathiri tabia ya watoto. Mama huyu alisema, *"Kwa hiyo sisi kuishi katika mazingira mageni sana kunaweza kukufanya ujisikie kwamba watu hawakuoni, bado hatujui jinsi gani mustakabali wetu utakuwa, kama vile kitu gani tunapaswa kubadili au nini kitabadili mitizamo yetu siku kwa siku. Lakini hatuishi katika mtazamo mzuri. Sisi ni wazaliwa wa kwanza; watoto wetu wanatakiwa kuja kushuhudia mabadiliko. Lakini hatufikirii hilo. Jinsi tunavyoishi ndivyo watoto wetu wataishi kwa njia hiyo hiyo, hivyo basi tunajikuta hatuna kitu. Sisi tunasema kwamba tunapaswa kubadilika sisi wenyewe kwanza na vizazi vyetu vijavyo. Ili waweze kuona kila kitu kimebadilika, lakini hakuna jambo kama hilo hivyo unaweza kukuta kila kitu kinafuata mkondo kutoka zamani kwa kufuata nyayo zetu. Ndio maana siku hizi tunalalamika kwamba watoto ni wakaidi. Ni sisi tunaoonyesha utovu wa nidhamu na watoto wetu wanaona hili kutoka kwetu. Watoto watafuata nyayo zile zile. Ndio maana, sisi wakubwa hatuna ushauri wa kuwapa ambao unaweza kuwasaidia. Labda tunapaswa kubadilika sisi wenyewe kwa jinsi hii".*

### 4.3.4. Nafasi katika jamii

Wazazi waliulizwa kuhusu nafasi yao katika jamii hasa kwa sehemu wanazoishi. Wengi ilikuwa ni swali gumu sana

kujibu, wengi walidhani ilimaanisha nafasi ya kuwa kiongozi wa mitaa, ambayo hawakuwa nayo. Wengi wao hawajihusishi na nafasi yoyote katika jamii, mama mmoja maskini sana akajibu,

*"Kwa kusema ukweli kuhusu nafasi yangu katika jamii, sioni kitu chochote. Sioni nafasi ambayo naweza kusema mimi ninajivunia, kila nafasi ni tatizo. Ukikimbilia kwa majirani ni tatizo, kwa jamaa ni tatizo, na pia kwa mume wako ni tatizo. Lakini mimi tu na kukabiliana nayo kwa sababu yamenizunguka".*

Baba mmoja alikuwa na mtazamo chanya zaidi juu ya nafasi yake, akiihusisha zaidi na dini yake. *"Katika jamii mimi nasaidia katika masuala ya dini kwa kuwafundisha watu juu ya kumtii Mungu na kufanya matendo mema ambayo yanamfurahisha Mungu, hivyo mimi daima husema hili kwa marafiki zangu au hata wageni kwamba Mungu anakupenda. Wewe una afya, na familia yako pia, hivyo basi jambo la muhimu ni kumtii Mungu".*

Ingawa watu waliohojiwa hawakuwa na rasilimali hivyo kuwa vigumu kusaidiana katika jamii yao hasa kifedha hata hivyo hushiriki katika kujenga na kuimarisha jamii wanayoishi. Kwa mfano, familia moja inayoishi katika eneo linalokabiliwa na mafuriko, ingawa hawawezi kuchangia kulipia mashine zilizokodiwa na wakazi, wao hujiunga na watu wengine katika kuchimba na kusafisha mifereji ya maji. Baba mwingine alikuwa muuzaji maji katika jamii yake, na kupitia kwa wateja wake aliunda mtandao mkubwa wa marafiki. Alipoanza kujihusisha na mradi wa usajili wa vizazi katika jamii yake, aliwaleta rafiki zake katika mradi na kusaidiana nao katika mchakato wa kusajili kuzaliwa kwa watoto wao.

### 4.3.5. Usiri na wivu

Hatua iliyojitokeza kwa nguvu sana katika utafiti ilikuwa ukosefu wa faragha hali ambayo watu maskini pamoja na familia zao hukabiliana nayo. Familia nyingi zilizohojiwa zinazoishi Tandale huishi katika mazingira ya kuchangia, ina maana wao huchangia sehemu kwa ajili ya kupikia na kufulia, na kutumia choo cha jumuiya. Kumiliki viwanja na nyumba binafsi kunaweza kuleta kiasi fulani cha faragha, ingawa siyo kwa ukamilifu.

Watu kadhaa walisema kuwa majirani *"kuchunguzana"* ilikuwa inakera na kuleta bugudha. Watu walizungumzia wivu kati ya majirani, kujua nani analala wapi, chumba gani, watu wangapi, n.k. Watu walikuwa makini sana hasa kuhusu kuchunguliwa wakati wanapopika na kula, kwa sababu aina ya chakula kinacholiwa na familia ni ishara ya utajiri, au ukosefu wa chakula. Baba mmoja alisema kuwa wivu unakuwepo kati ya majirani wakati familia moja inapoiona

familia nyingine inafanya vizuri, pale wanapokuwa na mafanikio na kuanza kujenga maisha yao, kwa mfano kuboresha makazi yao.

### 4.3.6. Mazingira

Walimu, wazazi na watoto wote walizungumzia kuhusu changamoto mbalimbali katika habari za mazingira ambapo wanaishi. Neno mazingira lilitumika kuelezea maisha ya nyumbani (makazi) mazingira, hali ya hewa, eneo hilo na mambo mabaya katika eneo hilo, kama vile wezi na makundi.

Mama mmoja alizungumza kuhusu hofu yake kwa watoto wake. Alisema kwamba binti yake mkubwa alijitolea kusaidia familia yake kwa kuuza mboga mboga, lakini yeye kama mama alikataa kwa sababu ana wasiwasi katika jamii yao kwamba mtoto anaweza kufanyiwa vibaya na wateja wasiokuwa waaminifu.

Baadhi ya familia zinazoishi katika maeneo ambayo hakuna umeme, wakimiliki samani chache au hawana kabisa samani kama vile meza au kiti nyumbani. Ukosefu huu wa rasilimali za msingi unaweza kuleta ugumu au isiwezekane kabisa, kwa watoto kufanya mazoezi ya nyumbani nyaakati za jioni.

Moja wapo kati ya changamoto zinazowakabili watoto nyumbani ni kelele, kutoka katika nyumba zao wenyewe, majirani na jamii kwa ujumla. Watoto wengi walisema kuwa kelele, hasa sauti kubwa ya muziki, hufanya iwe vigumu kwao kuwa makini na kazi za nyumbani walizopewa shule. Mtoto mmoja alisema, *"Kwa sababu ya kelele ni vigumu kusoma, unajiambia 'kesho', lakini kesho kamwe haifiki".*

Misukosuko nyumbani inaweza kuja kwa njia tofauti kwa watoto. Mtoto mmoja alisema yeye huambiwa na wazazi wake afanye kazi za nyumbani anazopewa shule kila siku jioni, lakini pale anapowaona rafiki zake wakicheza nje hawezi kusoma kwa umakini. Mtoto mwingine alisema kuwa wakati mwingine inakuwa vigumu kusoma kutokana na nyumbani kwao kuwa na ghasia.

Kuishi mbali na shule ni tatizo lililozoeleka kwa baadhi ya watoto. Wanaweza kufika shule wakiwa wamechelewa na kuchoka, hivyo kuwafanya *"Washindwe kuelewa kile mwalimu anachowafundisha"*. Kutembea katika mvua huleta matatizo. Mama mmoja alisema, wasiwasi wake ni hatari inayowakabili watoto kuvuka mto wakati umefurika maji Njia pekee iliyobaki ni kutembea umbali mrefu barabarani ambako kuna magari mengi na pikipiki. Watoto wanaweza kuchelewa, na nguo kulowa pamoja na vitabu. Wanaweza kusikia baridi kwa sababu hawawezi kukauka, ambapo inakuwa ni kikwazo kwao kusoma. Mama mmoja alisema

“watoto wangu hawawezi kusoma kwa sababu mazingira yamewafanya wawe hivyo”.

Tatizo lingine ni jinsi gani hali ya hewa huwazuia watoto kuwa makini shuleni.

*"Wakati mvua inanyesha usiku na wewe umelala inaingia ndani ya nyumba, huwezi kufanya kitu kwa sababu paa limeharibika. Wakati mtoto yupo shuleni na anaona upepo mkali unaoambatana na mvua, yeye huanza kufikiri 'Oh Mungu wangu, nini kitatokea, nitalala wapi kwa sababu nyumba yetu si imara'. Wakati mtoto anafikiria kuhusu matatizo yote ya nyumbani kwa undani yeye hawezi kuwa makini katika masomo yake".*

Tatizo lingine lililoripotiwa ni kuhusu mazingira ambayo watu wanaishi yanayopelekea kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza na uhalifu. Baba mmoja alielezea kuhusu familia zinazoishi katika nyumba zinazochangia vyoo. Baadhi ya watoto huenda choo bila kuvaa viatu na hivyo kuweza kuambukizwa maradhi. Takataka zinapokuwa haziondolewi vinyama haribifu, wadudu na mbu huweza kuzaliana na hivyo kuongeza kasi ya kuenea kwa magonjwa.

Wazazi, walimu na watoto wote walizungumzia kuhusu athari hasi za klabu za video katika elimu yao katika shule za msingi. Mwalimu mmoja alisema,

*“Kuwa wakati watoto wanapokuwa katika vibanda vya video huiona shule kama mahali pasipo na thamani".*

Katika maeneo mawili ya msingi ambapo utafiti ulifanyika zipo klabu za video, maduka madogo au mabanda ambayo huonyesha sinema. Baadhi ya watoto, mmoja mmoja au pamoja na marafiki, hutega shule na hutumia siku zao kuangalia sinema. Mara nyingi klabu hizo za video kuonyesha sinema ambazo hazilingani na umri sahihi wa watoto ambao wanaangalia, maonyesho ya ghasia ghasia na picha za uchi. Mzazi mmoja alisema kuhusu watoto wanavyojifunza kuiba fedha kutoka kwa wazazi wao kutokana na kwenda na kuangalia sinema katika klabu za video badala ya kwenda shule. Mama mwingine alisema kuwa watoto wanaweza kujifunza jinsi ya kuiba kutokana na kuangalia sinema za vurugu, tabia ambazo huiiga kwa vitendo.

Kiongozi mmoja wa serikali ya mtaa alisema yeye alitoa amri kwa mabanda ya video kutofunguliwa tangu saa mbili asubuhi hadi saa nane mchana, na watakapofungua saa nane machana watahitaji kibali ili kukomesha tabia ya watoto kwenda huko. Wale wamiliki wa mabanda ya video ambao hawakukubaliana na hili walipelekwa polisi.

Watoto wote waliohojiwa walisema vibanda vya video huleta madhara hasi katika elimu yao. Mifano ya kwa nini hili

hutokea ilikuwa; watoto wanapewa pesa na wazazi wao kwa ajili ya ada ya masomo au kununua chakula lakini badala yake walikwenda kuangalia sinema; kuangalia sinema wakati wa usiku sana kisha kushindwa kuamka kwa muda kwa ajili ya shule; kuangalia sinema humaanisha watoto hawafanyi kazi za shule; wakati wa mitihani watoto walishindwa kwa sababu walikuwa wakienda kwenye mabanda ya video jioni. Sinema zinazooneshwa katika mabanda ya video huonesha ukatili na picha za ngono; watoto wanaweza kujifunza tabia mbaya na matusi; mabanda ya video huhamasisha watoto kutoroka shule. Watoto walisema pia kwamba kupitia kuangalia sinema katika mabanda ya video waliweza kujifunza jinsi ya kuiba na kuwaibia watu. Mtoto mmoja aliwahi kuona mtoto mwingine akiiba Tzs 500 nyumbani ili aweze kwenda kwenye banda la video.

Ingawa watoto walikubaliana kwamba kwenda banda la video si vizuri kwa elimu yao, watoto wengi waliohojiwa, walipoulizwa kama wanakwenda kwenye vibanda vya video, karibu wote wakajibu, ndiyo.

Katika maeneo ambapo mahojiano yalifanywa, wazazi, walimu na watoto iliripoti makundi ya vijana ambao waliona kuwa chanzo cha matatizo katika baadhi ya jamii. Watoto wa Tandale waliripoti kushambuliwa na magenge ya wahuni na kuibiwa fedha au vifaa vyao vya shule kama vile mabegi na viatu. Watoto walisema wanahitaji daima kubadili njia zao za kwenda shule, si kupita katika vichochoro na sehemu ambazo wezi hujificha. Watoto walisema wameona polisi wakipambana na idadi kubwa ya watu huko mitaani. Siku moja, walirusha mabomu ya machozi kuwafukuza, jambo lililowatia hofu watoto na hivyo kuacha shule na kurudi nyumbani siku hiyo. Watoto walisema kuwa vijana wengi katika makundi huvuta sigara madawa ya kulevya, baadhi hujaribu kushawishi watoto kujaribu madawa ya kulevya na kujiunga na makundi.

Mtoto mmoja akatoa ushuhuda huu binafsi,

> *"Nilikutana na kundi moja wakati narudi kutoka shule siku moja, mmoja wao alikuwa na kisu, alitaka kunikaba, ikanibidi nikimbie. Haya ni mazingira yetu, inabidi nitafute njia mpya ya kwenda na kurudi kutoka shuleni, ni katika njia za mkato kutoka shule ambako makundi ya wahuni hujificha katika kona ".*

Makundi haya ya vijana pia ni wasiwasi mkubwa kwa wazazi. Walisema kujaribu kuwarubuni watoto kwa dawa za kulevya (bangi), fedha, hata ahadi za chakula, ambayo inaweza kuwaelekeza watoto katika jambo baya, pengine hata katika tabia za jinai. Wazazi walionyesha hasira zao wakisema wanahitaji msaada kutoka kwa serikali kukabiliana na tatizo la makundi. Mzazi mmoja alisema kwamba kuwemo katika makundi haya kunaweza kuleta hisia za kiburi kwa baadhi ya watoto, na hili ni tatizo kubwa.

Walimu walipoulizwa iwapo huchukua hatua yoyote wanapojua kuhusu watoto kujiunga na magenge, walisema kuwa huwaambia watoto wengine kwamba wanapaswa kusisitiza marafiki zao warudi shuleni. Walimu waliwasiliana na wazazi wa kila mtoto aliyejiunga na makundi.

Wajumbe wa nyumba kumi katika kila eneo wanapaswa kujua umri wa kila mtoto wa eneo lao. Kwa hiyo kama mtoto asipoenda shule, wajumbe wa nyumba kumi wanaweza kupeleke habari hii kwa viongozi wa serikali ya mitaa kwa mwalimu mkuu wa shule. Hata hivyo, mjumbe mmoja wa nyumba kumi alitoa taarifa kwamba kwa ajili ya watu kuhamahama katika eneo lake ilikuwa vigumu kuwatambua watoto wote.

Watoto waliulizwa kuhusu changamoto wanazopata wakati wa kwenda na kurudi kutoka shuleni. Kwa wale ambao huenda kwa basi wao wote walisema kitu kimoja kwamba makondakta hawawaruhusu kwenye mabasi katika nyakati za kazi kwa sababu wao hulipa nusu ya nauli. Hii ilimaanisha watoto wengi walilazimika kutembea, au kutumia muda mrefu kusubiri basi litakalowaruhusu kupanda. Wakati watoto wanaruhusiwa kwenye basi, walisema kwamba baadhi ya abiria hawakuwajali, pengine walisukumwa na kuumizwa. Watoto wengine walisema kuwa wanaogopa kuvuka barabara, hasa barabara kuu ambapo magari hupita kwa mwendo wa kasi.

Kwa wale watoto ambao wanaishi mbali na shule, wanaweza kupitia *"matatizo"* mengi ya kimazingira jambo linalowaweka katika hatari kubwa ya kukosa au kuacha shule. Mwalimu mmoja alizungumza kuhusu wasichana wadogo kupata mimba kama sababu ya kushindwa kumaliza shule ya msingi. Wasiwasi mmoja kwa wanafunzi wa kike ni makundi ya wanaume vijana ambao wanapishana nao wakati wa kwenda na kurudi kutoka shule. Walisema kwamba wakati mwingine hujaribu *"kuwavutia"* wanafunzi wa kike kuanza uhusiano nao.

### 4.3.7. Kuishi mahali pengine

Familia zilizohojiwa waliulizwa endapo walikuwa na fursa ya kuishi mahali pengine wangechagua kuishi wapi. Ingawa watu walitaka maisha bora na mazingira salama, hawakuwa wakifikiria kuwa kuishi mahali pengine itakuwa tofauti kuliko pale wanapoishi sasa. Wanajua kipato chao hakitoshi kuishi. katika eneo la kitajiri, lakini wao pia walikataa wazo hili kwa sababu walisema watu katika maeneo tajiri hawaishi kijamaa, wanaishi kila mmoja kivyake. Watu wote walioulizwa swali hili walisema wangeendelea kuishi walipo sasa kwa sababu wanao mtandao wa marafiki zao, ambao

wanaweza kusaidiana, na kwamba endapo wao wakihamia mahali pengine watakuwa wageni. Kuwa na mtandao wao ukiwa umewazunguka kunawapa usalama.

### 4.4 Kazi na kipato

Wazazi wana mambo mengi ya kusema kuhusu kiwango cha kipato chao. Hata hivyo ilitambulika na walimu kwamba kipato cha chini cha familia inaoishi katika umaskini ina athari mabaya katika elimu ya watoto. Mwalimu mmoja alisema,

> *"Kama mzazi hana kitu, hakuna fedha, wazazi wanaweza kuchukua watoto wao kufanya kazi pamoja nao, kama vile kugonga mawe".*

Kipato cha chini na kutokuwa na kazi maalum iliripotiwa na wazazi wote waliohojiwa. ukosefu wa usalama wa kazi, bila kujua ni kiasi gani anaweza kulipwa katika siku aliyopewa ni wasiwasi wa mara kwa mara kwa familiazinazoishi katika umaskini uliokithiri. Wengine walisema kwamba katika baadhi ya siku wao huwa na fedha tu ya kutosha kununua chakula. Mama mmoja alisema, *"Mimi sina hata pesa za kununulia mtoto wangu kalamu kwa ajili ya shule".*

Kawaida ya familia nyingi zinazoishi katika umaskini uliokithiri kwamba mara nyingi wanachokifanya ni kufanya uchaguzi kutokana na kile kipato kidogo walichonacho. Kuna baadhi ya familia wanao watoto zaidi ya mmoja wanaokwenda shuleni hivyo hulazimika kufanya uchaguzi ni yupi aende shule na yupi abaki nyumbani. Hii inaweza ikawa ratiba ya kudumu au siku kwa siku. Mama mmoja alituambia,

> *“Huwa nawambia wanangu sina hela, kwa hiyo baki nyumbani nikipata pesa leo utakwenda shule kesho”.*

Uchaguzi mwingine wanaolazimika kufanya ni kula mara chache kuliko inavyotarajiwa kiafya. Wengi walizungumzia kuhusu mlo mmoja kwa siku. Mara nyingine badala ya mlo kamili walikunywa chai au uji. Wazazi walielezea umuhimu wa kumpatia mtoto kifungua kinywa asubuhi, lakini wakati mwingine ufinyu wa fedha uliwasababisha kushindwa kutekeleza hili. Wazazi walisema mtoto anayetoka katika familia iliyo na uwezo na anapata kifungua kinywa uwezo wake wa kufanya vizuri shuleni unakuwa mkubwa.

Baba mmoja alielezea kuhusu njia mbadala ambayo angetumia kufanya kwa ajili ya elimu ya mwanaye endapo angekuwa na pesa ya kutosha. *"Nisingempeleka mtoto wangu shule za serikali, ningempeleka shule ya kulipia. Nikifanya kazi kwa muda wa mwaka mzima sipati pesa ya kutosha kumlipia shule ya kimataifa ya binafsi. Shule za*

*serikali sio nzuri, shule za binafsi ndipo unapompeleka mwanao ukiwa na pesa".*

Miongoni mwa wazazi waliohojiwa kumi ni wafanyakazi katika machimbo ya mawe Tegeta (Boko na Kunduchi). Baadhi ya wavunja mawe huajiriwa na waajiri wasio rasmi ambao huwalipa kwa kila ndoo wanayoponda. Siku nyingine wafanyakazi hawalipwi au wanalipwa kidogo sana. Mama mmoja alituambia *“Kuwa siku zingine silipwi, nitafanya nini, mawe hayawezi kukupa pesa”.*

Wazazi wote waliohojiwa walisema kazi zao ni muhimu kwa maisha. Siyo kwamba kazi yao ingekuwa chaguo lao la kwanza. Walisema kwamba kazi ni kile unachokifanya kupata pesa, shughuri ndogondogo za kila siku au biashara ndogo ndogo. Hizi shughuri ndogo ndogo ni kama vile kuuza mboga mboga na matunda, kusafisha samaki, kuponda kokoto n.k. Karibu wote huwategemea wateja, na kiasi wanachopata kila siku hutofautiana. Masuala mengine yanaweza kusababisha kupoteza pato, kama vile magonjwa katika familia. Mama mmoja alisema, “*Mwanangu anaumwa, siku hizi nabaki nyumbani, sipati pesa”. Mama mwingine aliulizwa iwapo anaifurahia kazi yake, alisema”Hiyo furaha inakujaje rafiki yangu, biashara ni ngumu, unatembea huku na kule hadi miguu inawaka kama vile kuna moto ndani yake. Lakini huna budi kuipenda, ukiikataa utakula nini wakati ndiyo kazi yako?*

Waliongelea kuhusu ndoto zao kuhusu kazi ambazo wangetamani kufanya. Walisema wangependa kumiliki duka dogo, kuwa wafanya biashara, madaktari, wauza nguo na wanasheria. Wazazi wengi walihojiwa walisema wangependa kumiliki biashara zao wenyewe. Waliendelea kusema kwamba kuwa na biashara zao kunaweza kutoa "*uhuru*" na "*kujitegemea*". Haiwezekani kusisitizwa umuhimu wa kuwa na uhuru na kujitegemea kwa kila familia. Wanaona kwamba kuwa huru kunawezekana kwa njia ya kazi na ajira binafsi. Kujiajiri ilikubalikana katika familia nyingi, pale inapokupatia uimara na kipato cha kutosha kwa mahitaji yako.

Watu wachache waliohojiwa walikuwa wameajiriwa. Mmoja aliyekuwa mlinzi, alitoa taarifa kuwa kampuni aliyokuwa akifanyia kazi ilikuwa ikipokea kiasi kikubwa cha fedha lakini kiasi alichokuwa akilipwa kilikuwa kidodgo mno. Hakuwa na mkataba, likizo, wala bima ya afya. Masaa ya kazi ni mengi kinyume na sheria ya kazi ya Tanzania. Anajua kwamba akitoa taarifa basi mwajiri wake atamfukuza kazi ingawa alikuwa anamnyonya. Kuwa na kiwango kamili kwa mwezi japokuwa ni kidogo kinanipa ulinzi kwa familia kuliko ile kazi niliyokuwa nayo kwanza ya kuuza maji.

Kwa sababu yakipato kidogo ninacho kipata huwa nakopa dukani, imekuwa nikawaida miyongoni mwa watu wanaoishi katika umaskini. Baba mmoja alisema napewa mkopo kwa sababu muuza duka anamjua huwa anapokea mshahara kila mwezi hata kama mdogo pale tu. Anapopokea

ankwenda kulipa deni, lakini katkikati ya mwezi anakwenda kukopa tena na mzunguko unaendelea.

Kipato cha chini kwa watu wanao ishi katika hali ya umaskini hupelekea kuishi katika hali za aibu. Baadhi ya wazazi wametueleza huwa wanakwenda kukopa dukani ili familia zao ziweze kula na muda mwingine kabla ya kulipa huongeza deni lingine. Hujisikia fadhaa pale deni linapokuwa halijalipwa, na anapolazimika kukopa humtuma mtoto dukani kukopa vitu vingine. Mama mmoja alisema mwenye duka alimuuliza mwanaye *“Kwa nini unakuja wewe? Wazazi wako wapi?”*. Mama huyu huyu alisema, *“Kama huna pesa aibu, kubwa”.*

Kuna aina ya kazi watu wanazozifanya huleta aibu. Baba mmoja mlemavu hawezi kufanya kazi ngumu, wakati alipokuwa mzima alifanya kazi ya kubeba sementi na kupata pesa zaidi kwa ajili ya familia yake. Mama mmoja anafanya kazi ya kutembeza mboga za majani na kuitilia *“mboga! mboga!”* Watu wengine husema *“kwa nini ana tuamsha asubuhi hivi na kazi yake?”*

Wazazi waliulizwa kama umaskini unaathiri elimu ya watoto wao Wengi wao walijibu “*Ndiyo*”. Wengi walihusisha umaskini uliokithiri na kutokuwa na kipato. Ingawaje wengine walizungumzia kukiukwa kwa haki zao, unyanyaswaji kutokana na kuwa maskini. Baba mmoja alisema “*Kama mtoto anaenda shule na sare zake haziko katika hali nzuri hunyanyaswa hata na watoto wenzake*”. Mama alisema

*“Ukiwa maskini hamna anayekuheshimu, huwezi kualikwa hata kwenye vikao vya kifamilia kwa sababu wewe ni maskini na kama utaalikwa basi kauli yako haiwezi kusikilizwa. ”Umaskini unashusha utu wa mtu hata ndani ya familia”.*

Kuhusu kipato kidogo hali hii mara kwa mara humtia hofu mama mmoja kuhusu maisha yake ya baadae katika familia yake. “*Muda wote nafikiria iwapo mwanagu atamaliza shule ya msingi kweli, nafikiria nirudi kijijini kwenda kuanza maisha mengine kwa sababu hapa mjini maisha ni magumu mno. Kwa hiyo mguu mmoja ndani, mguu mmoja nje inanifanya nisijue nini cha kufanya tena*”.

### 4.5. Afya

#### 4.5.1. Kuwa na afya

Kuwa na afya njema ni muhimu kwa maisha. Watu waliulizwa afya jema ina maana gani kwao. Baba mmoja alisema, “*Kwa mtazamo wangu afya ni hali ya mwili kuwa katika hali nzuri mara zote. Kwa sababu kama hauna afya nzuri huwezi kufanya kazi kwa sababu mwili unakosa nguvu. Kwa hiyo afya ni kitu chenye thamani sana kwasababu inawezesha kufanya vitu vingi sana, ikiwa*

*hauna afya inakuwa tatizo. Kuwa na afya ni faida kubwa katika mwili".*

Kuwa na afya kulihusishwa pia na mazingira ya familia. Baba mmoja alisema ni muhimu kuwa na kiti au kitanda nyumbani ambapo unaweza kupumzika wakati ukiwa unaumwa, alikuwa ana mkeka ambao alikuwa analala chini ya sakafu. Pia kuhusu afya mama huyu alisema *"Naweza kusema kuna afya ya mwili na afya ya kimazingira. Vyote ni kuhusu afya. Afya ni hali ya kula vyakula vyenye kujenga mwili au mtu anaweza kukuambia kuwa afya ni ile hali ya kuweka mazingira safi".* Mama mmoja alisema juu ya familia yake, kuwa na afya nzuri ni,

*"Kujenga mwili vizuri na kulala bila ya kuwa na mawazo au kuumwa kichwa."*

### 4.5.2. Kuumwa kwa watoto mashuleni

Wakati mwingine watoto wanumwa wakiwa shuleni. Inaweza kuwa ajali au kuumia, au kutokana na magonjwa kama pumu. Wazazi walisema kwamba kwa matukio kama hayo wanapaswa kuitwa shuleni.

Mama mmoja mwenye watoto wanne alizungumzia kitu kimoja muhimu kwa watoto wanapokwenda shule huku wakiwa wanaumwa. Alitoa mfano kwa mwanawe wa kike ambaye alikuwa akiumwa, alipewa dawa hospitali ambayo alimeza na kisha kuendelea kwenda shuleni kwa sababu hakutaka kukosa vipindi, ingawa ilikuwa ni vigumu sana kwake kusoma akiwa shuleni kwa siku zote kwa sababu hakuweza kufuatilia vizuri masomo na dawa zilikuwa kali sana kwake. Suala hilo hilo lilielezwa kuhusiana na watoto wenye matatizo ya macho. Iwapo hawataweza kuona katika ubao wakiwa darasani, hii inaweza kuwazuia kusoma vizuri.

Watoto walitaarifu kwamba wanapokuwa wagonjwa hukukaa nyumbani hivyo kukosa masomo shuleni, jambo ambalo linaweza kusababisha kutofanya vizuri katika mitihani. Ugonjwa kuwa mkubwa na watoto kukaa nyumbani kwa muda mrefu kunaweza kuwa tatizo kubwa la kukosa kufanya kazi za shule. Watoto walisema walimu wanapaswa kufikiri juu ya watoto ambao ni wagonjwa sana na hukaa nyumbani kwa muda mrefu. Wakati mtoto anarudi tena shuleni baada ya kuumwa, walimu waliwaambia waazime madaftari kwa watoto wengine na kunakili kazi na kushika haraka. Watoto maskini walisema kwamba mara nyingi watoto wengine waliwakatalia ombi lao. Mtoto mmoja alisema kuwa wakati yeye anarudi shuleni baada ya kuumwa, mwalimu wake humsaidia kumuelekeza yale ambayo aliyakosa.

### 4.5.3. Ambapo wazazi wanaumwa

Afya ya wazazi ni muhimu sana kwa kuhakikisha watoto wanakwenda shuleni. Hii ni muhimu hasa kwa mtu ambaye familia inamtegemea kwa kupata fedha kutoka kwake. Wazazi wanaposhindwa kufanya kazi kwa sababu ya kuumwa, kunakuwa hakuna kipato na watoto wanashindwa kwenda shule. Pia, kama mtu mzima anaumwa ambaye jukumu lake ni kuamsha na kuandaa watoto kwenda shuleni, inakuwa ni vigumu kwa watoto kuweza kwenda. *"Ikiwa kuna mtu anaumwa katika familia yangu, pesa ninayokuwa nayo inatumika kumpeleka hospitali, kisha watoto hukosa pesa ya nauli kuwapeleka shuleni".*

### 4.5.4. Gharama za matibabu

Wazazi waliohojiwa walikuwa na mengi sana kuelezea kuhusu pesa na afya. Eneo moja lililozungumziwa ni kwamba mmoja wa wanafamilia anapoumwa pesa inahitajika katika ulipaji baadhi ya matumizi hospitalini, matibabu, ushauri wa daktari kununua dawa n.k. Hii ndio pesa na muda mwingine unaweza kuwa hauna. Mama mmoja alisema ni kawaida kwa watu maskini kukaa na ugonjwa kwa sababu hawana pesa ya matibabu. Wazazi wengi wametaarifu kuwapatia watoto Panaldo, ili kutuliza maumivu. Ni njia pekee wanayoitumia wanapokuwa hawana pesa ya kumpeleka mtoto hospitali.

Wakati familia zinazoishi katika umaskini zinapokuwa hazina pesa ya kumpeleka mtoto hospitali na wanapohisi kuwa ni dalili za ugonjwa fulani, hutumia dawa za asili za mimiea. Hii inaweza kuwa ni sehemu ya kutumia kiasi kidogo cha pesa lakini pia kutokuwa na imani katika dawa za kisasa. Katika familia moja, mama anao ufahamu mkubwa wa dawa za asili na mahali zinapatikana

Tatizo lolote lile linalohusiana na ugonjwa huwa linahusishwa kwa karibu mno na upatikanaji wa pesa. Familia inapokuwa na kiasi kidogo cha pesa, huchukua nusu ya dawa walizoshauriwa kuchukua. Ikiwa ni dalili ya malaria au ugonjwa wanoufahamu, mara nyingi wazazi hawaendi kupima wala hata kuwapeleka watoto wao hospitali, badala yake huenda moja kwa moja duka la dawa na kununua dawa kupunguza gharama ya pesa iliyopaswa kutumika kupima.

Familia zilizohojiwa walisema ilikuwa ni kawaida ikiwa mtu anaumwa sana katika familia na dawa zake ni ghali sana, kuchukua baadhi ya vitu vya ndani na kuuza ili aweze kupata matibabu. Gharama za matibabu kwa kawaida huwa jukumu la kila mmoja katika familia. Hakuna familia hata mmoja iliyohojiwa iliyotaarifu kuwa hupata msaada kutoka kwa majirani na wengi walisema kuwa ndugu zao walikuwa hawana uwezo wa kulipa gharama za matibabu. Hakuna familia hata moja iliyohojiwa iliyotaarifu kuwa na bima ya

afya. Baba mmoja tu aliripotiwa kuwa anahifadhi kiasi kidogo cha pesa kwa ajili ya dharura.

#### 4.5.5. Maombi

Mara kwa mara tena, familia zote waliohojiwa walisema, wanapokuwa na afya dhaifu huwa *“wanamuomba Mungu”*. Kumuomba Mungu ilikuwa ni hatua ya kwanza, labda pale mzazi au mtoto anapokuwa amezidiwa sana ndipo hutumia dawa au humpeleka hospitali. Kati ya waislamu na wakristo waliohojiwa walisema huwa wanamuomba Mungu wanapokuwa na afya nzuri na hata wanapokuwa wanaumwa ili waweze kupona.

#### 4.5.6. Kwenda hospitali

Umbali wa vituo vya afya umezungumziwa na familia zilizohojiwa. Watu wote wanaoishi Tandale huenda hospitali ya Tandale au huamishiwa hospitali ya Mwananyamala. Wale wanaishi maeneo ya Tegeta huenda katika zahanati na ikiwa wamezidiwa sana pia hupelekwa hospitali ya Mwananyamala.

Wazazi walielezea uzoefu wao wa kwenda hospitali. Kitu kilichopo wazi ni kwamba ukiwa maskini inapunguza ubora wa huduma ya afya ambayo ungepaswa kupatiwa. Mama mmoja alisema,

> “*Kama ningekuwa na pesa nisingehudumiwa vibaya”.*

Rushwa na mapokezi mabaya hospitalini kwa watu wanaoishi katika umaskini hali hii iliripotiwa kwa kila mtu aliyehojiwa. Wazazi hawakuwa na matumaini kwenda hospitali. Ilikuwa ni kawaida kusema, ikiwa mtu anaumwa huenda hospitali kwa kutarajia kuhudumiwa na kupata nafuu lakini huduma imekuwa hafifu. Watu wanaojaribu kukutana na daktari bila ya pesa hurudishwa. Watu hupoteza tumaini na kukata tamaa. Watu wengi hurudi nyumbani bila ya kumuona dakatari au kutotibiwa.

Tanzania huduma ya afya kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano ni bure. Ingawaje katika sehemu nyingi wazazi wametueleza kuwa inawagharimu kulipia huduma kwa watoto na kila wakati hospitali wanasema hawana dawa ambapo inawagharimu kununua dawa katika maduka ya dawa yaliyo karibu na hospitali. Aidha kwenda hospitali au katika maduka ya dawa ya watu binafsi, mara nyingi maduka ya dawa hayana dawa sahihi zilizoandikwa na daktari. Inapotokea hali hii badala yake hupatiwa panadol.

Kunyanyaswa hospitalini inaweza kuwa kwa maneno au vitendo. Mama mmoja alifukuzwa hospitalini kama *“mnyama”* mwingine alisema alihudumiwa kama *“Mchawi”*. Mama mwingine alisema *“Nilipoona kuwa viti vya kukalia vimejaa, nilipanga foleni na mwanangu. Sitosahau nilivyoambiwa maneno mabaya nikiwa na mwanangu”.*

Siku nyingine hospitali mama huyo huyo *“Hivi karibuni niliambiawa kipimo kimoja kinaghalimu shilingi elfu 40,000/- na kingine ni elfu 15,000/- nilikaa kimya na sikumuuliza kitu chochote daktari, lakini alianza kusema maneno mabaya kwangu, nakumbuka nilikaa kimya. Nilijaribu kumuomba aniandikie majibu yangu kwenye karatasi ili nikatafute pesa ili nije kulipa”.* Aliendelea kuzungumzia kuhusu hospitali *“Siku hizi wanahitaji watu wawe na bima na sio sisi watu wa hali ya chini”.*

Wazazi walikuwa na uzoefu tofati wa sehemu za kutolea huduma za afya. Kila mzazi alisema wanamjua daktari gani “*anayewajali*” na kuwasaidia wagonjwa. Baba mmoja alisema muda mwingine unaweza kukutana na “*msamalia mwema*” akakusaidia, daktari au msaidizi wa daktari ambaye kweli anawajali wagonjwa. Mama mmoja kwake ilikuwa ni vizuri, alisema kuna baadhi ya siku huduma zilitolewa vizuri sana.

> *“Kuna changamoto nyingi sana. Muda mwingine unapokwenda wanakutibia vizuri sana na unahisi umeridhika, kwa hiyo huwezi kusema wanafanya vibaya kila siku. Siku zinakuwa tofauti na inategemea na mtu, baadhi ya watu wana moyo wa kusaidia. Ndio maana unaweza kukutana na mtu anasema kwamba, nikimkuta dada yule kazini nahudumiwa vizuri sana, sio kama wengine. Kwa mfano, kuna nesi mmoja, ikiwa yupo katika zamu siku hiyo huwa hata sisikii uchovu kupanga foleni kwani najua ikifika zamu yangu ninapata hudumu nzuri. Kwa hiyo tunapaswa kuwashukuru wote walio na moyo mzuri ambao wapo tayari kutusaidia na sio kuwalaumu tu”.*

Wakati wa mahojiano mama mmoja alielezea kwamba ikiwa mtoto akipata ugonjwa akiwa shuleni anaweza kupelekwa hospitali na akatibiwa bure, kwa kuelewa kuwa ugonjwa umempata akiwa shuleni na ameandikwa katika daftari la shule. Juu ya hili alisema, “*Wanaporudi kutoka shuleni wakati wanaumwa huwa ninampa Panaldo kwa sababu ukienda hospitali unakaa sana kwenye foleni. Shuleni wanacho kitabu chao cha usajili. Hata hivyo, najisikia kama usumbufu kuwaomba kitabu cha usajili. Binafsi sijawahi kufanya hivyo huwa ninampa panaldo na dawa za malaria*”.

Katika vituo vya afya wazazi walisema kwamba “uongozi mzuri” na “*ukaguzi wa mara kwa mara*” unaoendeshwa na serikali ni muhimu na unaleta maendeleo. Pia mahospitalini kupatikana dawa ni hatua kubwa sana ya kuwa na huduma ya afya nzuri. Mwishoni mama mmoja alielezea vizuri kitu gani kingeweza kuboreshwa kwake wakati anapokwenda hospitali, “*Kitu ambacho kingepaswa kuboreshwa katika huduma ya afya ni kuondosha usumbufu wakati unapofika hospitali*”.

### 4.6. Shule

Elimu nzuri ilichukuliwa kama kitu kinachoweza kupatikana na ilikuwa inakaribishwa. Wazazi walikuwa na uhalisia na walisisitiza umuhimu wa shule kuwa na mazingira tulivu ambayo ni mazuri kwa ajili ya kujifunza. Ndoto ya wazazi wengi ni kwamba watoto wao waweze kwenda mbali zaidi kielimu, kufikia kiwango bora zaidi kuliko wao, kutambua hili kunaweza kufungua uwezekano katika siku zijazo ambako wao hawakuweza kufikia. Elimu ni kuhusu *"Kupata uelewa wa maisha"* Mama huyu alisema,

> *"Elimu bora kwa ajili ya mwanangu ni kuishi nyumbani katika mazingira mazuri na kuwa na mazingira karibishi shuleni. Walimu kumfundisha vizuri na awe anaelewa. Hiyo ni elimu nzuri".*

#### 4.6.1. Juhudi za wazazi, watoto na walimu

Mahusiano kati ya wazazi na walimu wakati mwingine huweza kuwa magumu, yenye changamoto, na katika baadhi ya mazingira, kuvunjika kabisa na kusababisha hasara kwa elimu ya mtoto. Hata hivyo utafiti uliofanyika, ulileta ugunduzi wa mambo mengi chanya ambayo lazima yatiliwe maanani ili kuleta hamu ya mahusiano bora na ushirikiano uliopo.

Wazazi waliongelea juhudi wanazofanya hasa kuhusu ufuatiliaji wa elimu ya watoto. Wazazi walitambua kwamba watoto wanayo mahitaji ya nyumbani na shuleni ambayo yanapaswa kutimizwa ili kuhakikisha mafunzo imara. Nyumbani mahitaji hayo ni pamoja na kwamba mtoto kupata kifungua kinywa kabla ya kwenda shule, sare safi, madaftari na kalamu, na kutiwa moyo na wazazi.

Watoto wanaporudi kutoka shule, wazazi huandaa chakula, huhakikisha watoto wanabadili nguo zao na kuangalia kazi za shule. Hizi ni baadhi ya njia ambazo wazazi hutumia kuwahamasisha watoto wao kufanya bora katika shule.

Nyumbani wazazi walisema jinsi gani ni muhimu kuangalia madaftari ya mtoto, lakini kwa baadhi ya wazazi ambao hawawezi kusoma na kuandika hii haiwezekani na inaweza kuwafanya wao kujisikia aibu. Mzazi mmoja alisema katika mazingira kama hayo wazazi wanapaswa kutafuta njia nyingine ya kuwatia moyo watoto wao katika masomo yao, ambayo inaweza kuwa pamoja na kuangalia madaftari na kuona kama walimu wamesahihisha kazi au kuuliza wanakaya wengine kumsaidia mtoto. Mama mmoja alisema kwamba kaka mkubwa, ambaye amemaliza elimu ya sekondari alikuwa na uwezo wa kumsaidia ndugu yake mdogo kazi za masomo ya nyumbani ambazo mama yake hakuweza kumsaidia. Mama mwingine alisema ingawa hakuweza kusoma na kuandika yeye alikuwa na uwezo wa kutambua alama za walimu au makosa katika madaftari na

kuelewa kama mtoto alikuwa akifanya vizuri au si katika masomo.

Kuwa karibu na watoto kulisisitizwa na wazazi. Baba mmoja akasema yeye hupata muda wa kumuuliza mtoto wake kama wana matatizo yoyote na anamsikiliza, na kama anaona mtoto anakabiliwa na changamoto yeye hufanya ufuatiliaji.

Mzazi alisema, *"Mtoto anaporudi nyumbani kutoka shule, angalia daftari la mazoezi kuona endapo alifanya vizuri au vibaya. Mwambie mtoto, 'Hapa umefanya vibaya, lakini hapa umefanya vizuri sana. Ongeza juhudi zako mwanangu, kesho utakuwa juu'. Lazima kuwapa faraja watoto. Si vizuri wakati ukiona makosa kidogo kupiga kelele na kumwadhibu mtoto. Usiseme, 'Mimi ninakupa fedha na anafanya vibaya'. Hii inamfanya mtoto kujisikia vibaya. Lazima kumhimiza mtoto wako, kuhamasisha juhudi za mtoto".*

Baba mmoja aligundua njia ya kumhamasisha mtoto wake katika masomo yake, alisema, *"Mimi hutumia muda wangu kunakili maswali katika kitabu chake cha shule kwenye karatasi tofauti, basi mimi humuuliza maswali tena na yeye hujibu. Kwa njia hii, haya ni mazoezi mazuri, lakini huweza pia kutambua kwamba yeye hajanakili kutoka kwenye daftari la mtoto mwingine".*

Wazazi wengi walisisitiza kutokuwa na muda wa kuwa karibu na mtoto wako kutaathiri na kuharibu elimu yake. Mzazi mmoja alisema. *"Unahitaji kuwa bega kwa bega na mtoto wako".* Mzazi mwigine alisema watoto wanahitaji *"Tabia nzuri ya kuhudhuria shule",* hasa kupata msingi bora wa elimu ya msingi.

Watoto waliulizwa kuhusu juhudi zao katika masomo yao. Watoto wote walisema kusoma kwa bidii na kujaribu sana ni jambo la muhimu, ambalo linaunganishwa na mitazamo yao juu ya umuhimu wa elimu, kwamba kufanya jitihada sasa kutawasaidia wao na familia zao katika siku zijazo. Watoto pia walisema ni muhimu kuwasikiliza walimu na kuwa na ratiba nyumbani ambayo inakupa muda wa kusoma. Kuhamasisha marafiki kusoma kwa bidii pia kulionekana kama moja ya juhudi ambazo watoto hufanya shuleni ili wafanikiwe.

Watoto walisema kuwa watu tofauti walihusika katika kuwasaidia wanaporudi nyumbani kutoka shule, ikiwa ni pamoja na wazazi, babu na bibi, ndugu wakubwa, majirani, na kila mmoja. Baadhi ya watoto walisema walikuwa na jirani ambaye alikuwa mwalimu na waliweza kwenda kuomba msaada kwake baada ya shule. Kusaidiana ilikuwa kawaida miongoni mwa watoto, mtoto mmoja alisema, *"Rafiki yangu ambaye yupo darasa la juu hunisaidia mimi, sisi tunakaa pamoja nyumbani na yeye ananisaidia".*

Kuhusu umuhimu wa shule mtoto mmoja alisema:

> *"Elimu ni muhimu kwa sababu kupitia hiyo naweza kufikia ndoto zangu; elimu ni muhimu kwa maisha yangu, mimi nikiwa mkubwa nitaweza kuwasaidia wazazi wangu. Elimu hutoa mwongozo kwa maisha yetu ya baadae"; "Kama utakosa elimu inaweza kuwa sababu kubwa ya umaskini"* na *"Elimu hunisaidia kufikia malengo yangu. Elimu ni ukombozi kwa maisha yangu, familia yangu na kwa jamii yangu".*

Hata hivyo, kwa baadhi ya watoto kutoka familia maskini sana wao kuweka juhudi zao lakini wanahisi kutofanikiwa chochote. Mtoto mmoja anayeishi katika eneo la Tandale ambaye alikuwa na historia mbaya sana alipokuwa shule ya msingi, alisema, *"Naona elimu ni muhimu, lakini pia si muhimu. Kati ya wale wanaokwenda shule na wale ambao hawaendi shule naona hakuna tofauti. maisha yao ni sawa. Mimi mwenyewe niliamua kuacha kwenda shule kwa sababu tulikuwa tunahama hama sana na sikuwa na fomu za uhamisho hivyo sikuweza kusoma, hivyo hakukuwa na ulazima wa kuendelea kwenda shule. Tuliporudi Dar mimi nilisajiliwa kwa darasa la Memkwa na watoto wadogo kuliko mimi, nilikuwa katika darasa moja na mdogo wangu wa kike lakini mimi nikiwa mkubwa. Kwa kuwa nilikuwa mkubwa katika darasa nilijiona mjinga, nilikuwa najua kusoma na kuandika lakini waliendelea kuniweka katika darasa hili. Hii ndio sababu ya kuacha kwenda shule".*

Walimu wanatumia juhudi katika kuboresha elimu ya watoto pamoja na kutumia vifaa vya kufundishia vilivyotolewa, kwa kufuata mitaala na kutumia mbinu nyingine ambazo wamezipata kutokana na uzoefu wa miaka mingi wa kufundisha watoto.

Mwalimu mmoja alisema,

> "*Walimu wanapotumia mbinu nzuri za kufundishia na vifaa huwahamasisha watoto kuwa wabunifu na kusoma kwa bidii, na kwa njia hii watoto kuhamasishana kila mmoja kuendelea zaidi katika masomo yao. Ikiwa watoto wanafurahia walimu wao na kushirikiana katika njia nzuri, hii huleta hamu zaidi ya kujifunza kwa ngazi nyingine".*

Mwalimu mwingine alisema kama watoto wanaweza kuona nini wanaweza kufikia ni sawa na mwalimu, wataona watamwona uyeye kuwa sawa na wao. Huyu mwalimu alijaribu kuhakikisha kuwa hakuna matabaka yaliyokuwepo kati yake na watoto.

Juhudi za walimu kufika mapema na kuwakaribisha watoto katika njia nzuri, huwahamasisha watoto wadogo kufika kwa wakati na kufuata mfano mzuri wa walimu. Walimu pia huwahimiza watoto kuuliza maswali darasani na kuweka juhudi zao binafsi. Mwalimu alisema, *"Elimu ni muhimu kwa sababu watoto ni kizazi cha baadae cha taifa letu".*

Mwalimu mmoja alisema, *"Serikali, kamati za shule, walimu na wazazi kila mmoja wana wajibu wa kuhakikisha watoto wanapata elimu ya msingi. Kwa serikali kujenga miundombinu na vifaa, kwa walimu kutumia vifaa hivi ili kutoa elimu, kwa kamati ya shule ili kupata wadau wengine katika jamii ili kusaidia shule, na kwa wazazi kutoa sare, madaftari na kalamu".*

Mazingira ya shule yanapokuwa ya kuvutia, watoto huwa na hamu zaidi ya kuja shuleni. Mwalimu mkuu alisema,

*"Shule ni mahali ambapo mtoto anapaswa kufurahia kupata elimu. Shule binafsi zinakuwa na vifaa kamili na nyenzo zote, hii ina maana kwamba watoto hawa watafanikiwa, ambapo shule za serikali hukosa fedha za kununua vinavyohitajika katika kuelimisha watoto. Inakuwa vigumu kuongoza shule kukiwa na uhaba wa fedha",* alisema mwalimu mkuu.

#### 4.6.2. Ushirikiano

Wazazi na walimu kwa pamoja wote walisema kwamba ushirikiano mzuri kati ya pande zote mbili ni sababu kubwa kwa watoto wao kuweza kuhitimu shule ya msingi. Upo utashi mkubwa katika kushirikiana na walimu kwa kuwa wazazi wanafahamu kwamba hii itawafaidisha watoto katika elimu na itawaondolea baadhi ya mashaka yao. Mama mmoja alizungumzia kuhusu hofu yake ya kila siku,

*"Mpaka wakati wtoto wake wanaporejea nyumbani ndipo wakati unapoweza kuwa na amani"*.

Kufahamu utaratibu wa mtoto ni muhimu, kujua wakati wa mtoto kwenda shule au kurudi nyumbani kunaweza kupunguza wasiwasi wa mzazi. Kama mtoto huchelewa kwa kuwekwa shule masaa mengi, au mara kwa mara hurudishwa nyumbani mapema, wazazi hukosa uhakika wa mara kwa mara wa ratiba ya shule. *"Mimi kushirikiana nao (walimu) juu ya masuala ya kitaaluma. Wakati fulani niliongea na walimu kuhusu suala la mtoto wangu kurudi nyumbani bila madaftari yake kusahishwa, mimi nilifanya ufuatiliaji mpaka madaftari yakaanza kusahishwa".*

Wazazi walisema walimu wanapofahamu mazingira kwa upana kuhusu familia na mazingira makazi ya watoto hii kuleta uelewa mzuri kwa ajili ya mahitaji ya watoto maskini wa elimu na changamoto. Mama mmoja alizungumzia kuhusu binti yake kurudishwa nyumbani kwa sababu hakuwa na fedha za kulipia ada ya mitihani ya majaribio. Alikwenda shuleni na alizungumza na mwalimu na mwalimu mkuu na akasema kwamba binti yake aruhusiwe kurudi shuleni na kujifunza mpaka yeye atakapokuwa na fedha za kulipia, jambo ambalo walimu walilikubali. Mama huyu tayari aliwajua walimu kwani kabla, yeye alikuwa akiitembelea shule mara kwa mara kufuatilia maendeleo ya mtoto wake.

Bila misingi hii mizuri ya mawasiliano ya wazi kwa wake, ushirikiano huu na walimu usingewezekana.

Mama mwingine alizungumzia kuhusu uzoefu wake kwamba mtoto wake asipohudhuria shule, yeye huitwa na mwalimu ambaye humuuliza kwa nini hakuhudhuria. Alisema huu ulikuwa ushirikiano mzuri kutoka upande wa shule na alihimiza ari ya mbinu hii.

Kupata taarifa ya maendeleo ya elimu ya mtoto ni muhimu kwa wazazi wanaoishi katika umaskini uliokithiri, hasa kama mtoto hafanyi vizuri shuleni. Kama mtoto anakuwa na udhaifu katika uelewa katika kusoma na kuandika ni lazima kumuwahi mapema. Wakati tatizo limetambuliwa, wazazi wanapaswa kuwa na taarifa ili ufumbuzi uweze kupatikana na walimu kushughulikia suala hilo. Kuzungumza na walimu pia ni nafasi kwa mzazi kueleza kuhusu mtoto wake, kwa mfano kama mtoto anaweza kuwa na matatizo fulani kama si kusikia vizuri au matatizo ya macho. Kuwa na msongamano wa watoto darasani, inaweza kuwa vigumu kwa walimu kutambua mahitaji ya kila mtoto, jambo ambalo lilisisitizwa na wazazi wengi.

Kufuatia mada iliyozungumzwa na wazazi wote, viongozi wa serikali za mitaa walisisitiza umuhimu wa wazazi kufanya ufuatiliaji wa watoto wao. Mawasiliano mazuri kati ya wazazi na watoto yanaweza kuonyesha matatizo na ufumbuzi unaweza kupatikana. Kiongozi mmoja alibainisha,

*"Wazazi wanajaribu kadiri iwezekanavyo kufanya ufuatiliaji na kuwasiliana na walimu na viongozi wa serikali za mitaa".*

Kiongozi mmoja alitoa mfano wa kushirikiana na mzazi ambaye alikuwa anakuja kwake kwa ajili ya msaada. Mtoto wa mzazi huyu alikuwa anafanya utoro na watoto wengine, hivyo kiongozi huyu na mzazi wakaenda mahali ambapo walihisi wangemkuta, wakawakuta huko na kuwapeleka shule. Katika tukio lingine kiongozi huyo alishuhudia mtoto mwingine mara kwa mara akiwa haendi shule. Aliwasiliana na mzazi wa mtoto huyo ambaye alikuwa hajui hali hii na kuipatia ufumbuzi.

Wazazi wengi walisema kushirikiana na walimu wa mtoto wao ni muhimu lakini kwa sababu tofauti hawafanyi hivyo, kama yalivyoelezwa baba huyu *"Wazo zuri ni kuwa na mwalimu wakati wote ili kusaidia maendeleo ya elimu ya mtoto wako".* Hata hivyo, ingawa baba huyu alisema lilikuwa *"wazo nzuri"* alisema yeye mara chache huenda shuleni.

Wazazi wachache sana walielezea kuhusu kwenda shule kwa ajili ya kufutilia maendeleo ya mtoto. Walisema kawaida huitwa na walimu kwenda shule mara tu wanapohitajika kulipa ada. Wazazi wengi walisema mara zote huitwa shule katika suala la pesa, na kwa sababu ya kiwango chao cha chini cha kipato mara nyingi hawana fedha za kulipia michango wanapoambiwa kulipa.

Walimu walisema ushirikiano na wazazi upo, lakini ulisemekana kuwa *"mdogo sana".* Walimu walisema wanaamini kwamba iwapo ushirikiano kati ya wazazi na walimu utaboreshwa, kiwango cha elimu kwa wanafunzi kingeongezeka. Walimu huakikisha kwamba taarifa zote za mikutano zinawafikia wazazi.

Mwalimu mmoja alidadavua kwa kusema kwamba 75% ya wazazi hushirikiana na walimu, wakati 25% ya wazazi hawana ushirikiano katika shule yake. Aliendelea kusema, *"Kwa hao 25% ni wale ambao hawaji wakati wewe umeagiza waje, ukijaribu kufuatilia utagundua kuwa hawa ni wale wanaoishi katika umaskini".* Mwalimu mwingine alisema, *"Wakati mwingine maisha ya wazazi yanafanya kuwa vigumu kwao kuwa na ushirikiano mzuri na shule za watoto wao".* Hii ilithibitishwa na mwalimu mwingine ambaye alisema 35% tu ya wazazi walikuja kwenye mikutano ya wazazi na walimu. Alipoulizwa maoni yake ni kwa nini, alisema wazazi hawakuja kwa sababu ya *"ugumu wa maisha"*.

Walimu walikuwa wakweli katika ufahamu kwamba wazazi wengi hujishughulisha na biashara ndogo ndogo kwa ajili ya kupata mapato na kwamba endapo wazazi wataacha shughuli zao hizo watapoteza mapato yao. Hii inafanya kuwa vigumu kwa wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao, pamoja na kushirikiana na walimu, sio kwamba wanapenda iwe hivyo.

Walimu wengine walisema kuwa hakukuwa na ushirikiano imara na wazazi. Watoto wakiambiwa wawaambie wazazi wao waje shuleni au wanapewa barua wapeleke nyumbani, lakini wazazi wanashindwa kufika shule. Kama hali hii ikitokea walimu huiomba serikali ya mtaa kusaidia kutafuta hao wazazi.

Kushiriki mikutano ya wazazi na walimu inaweza kuwa hatua ya kwanza kuelekea kujenga na kuhimiza uhusiano mzuri kati ya wazazi na walimu. Wazazi walisema ni muhimu kuhudhuria mikutano hii ili kupata habari na kukutana na walimu. Pia ilikuwa ni fursa kwa wazazi kuhoji walimu au mwalimu mkuu katika masuala fulani. Mama mmoja akasema, *"Unapokuwa pale unachangia kitu, jambo ambalo linafanya mikutano hii kustahili kuhudhuriwa".* Kiongozi wa mtaa alisema, *“kamati ya shule ni kiungo kati ya shule na wazazi. Wajumbe wa kamati wanapaswa kupatikana kwa ajili ya wazazi. Hata hivyo nyakati zote sivyo ilivyo kwa kuwa wajumbe wanakuwa na shughuri zingine”*.

Hata hivyo, wazazi walijihisi kufadhaika kwa sababu hawakusikilizwa au mabadiliko waliyoyataka hayakutekelezwa. Baba mmoja alisema,

> *“Nadhani kuwa moja kwa moja hakuna mabadiliko kwa sababu yale yanayosemwa hapo, yanasemwa wakati uko pale, lakini usipokuwepo hakuna mtu wa kutekeleza mabadiliko".*

Mama wa watoto watano, wawili ambao wanahudhuria shule ya msingi, alitoa majibu kwa swali aliloulizwa endapo yeye anahudhuria mikutano ya walimu na wazazi, *"Mimi kuhudhuria nasema kweli! Mimi nilihudhuria mara mbili tu, baada ya hapo sikuhudhuria tena. Kusema kweli, wakati sisi wazazi tulipoitwa kwa mara ya kwanza kila mzazi alichanganyikiwa"*.

Hii mifano miwili ni kuonyesha kwamba wazazi wanataka kuhudhuria na kuchangia katika mikutano lakini maoni yao yasiposikilizwa na maamuzi kuchukuliwa kinyume, hupoteza matumaini kwamba ushiriki wa dhati unawezekana.

Wazazi waliongelea kuhusu udhalilishaji wanaoukabili wanapokwenda shule. Iliripotiwa kuwa walimu wanawalaimu wazazi kwamba hawawajali watoto wao. Kutokana na mazingira duni ambayo familia zinaishi, walimu huona hii kama moja ya sababu za watoto kuwa na utendaji duni shuleni.

Huu ni uzoefu wa mama mmoja katika kukabiliana na walimu. *"Ni aibu mno kwenda kuzungumza na walimu kwa sababu ya maneno wanayokwambia. Mwalimu mmoja aliniambia, 'kwamba hilo ni jukumu la kuwa na mtoto', mwingine aliniambia 'kwamba hayo ndiyo matokeo ya kumlea mtoto kama mzazi mmoja'. Hayo yalikuwa maneno toka kwa mwalimu mkuu! Hivyo haina maana kwenda kuzungumza nao".*

Haikuwa tu walimu pekee waliowasema wazazi. Kiongozi mmoja wa serikali ya mtaa alisema nimewaona baadhi ya watu *"wanaojifanya"* kuwa wao ni maskini ili wasilipe michango ya shule.

Walimu wengi walisema kuwa upo uhusiano wa wazi kati ya umaskini na watoto kushindwa kufanya vizuri katika elimu ya msingi. Hata hivyo, walimu wawili walipinga bila ya wasi wasi maoni ya wazazi. *"Tunawaomba wazazi kuchangia 10,000 kwa mwezi kwa ajili ya uji na wazazi hutuambia ni vigumu kwa wao kulipa fedha hizo, lakini unaweza kuona wao wanakwenda saluni kwa ajili ya kutengeneza nywele, au kwenda kunywa pombe katika vilabu. Hawawezi kuwachangia watoto wao lakini wanaweza kujifanyia yao wenyewe"*. Mwalimu mwingine alisema, *"Kuna watu wanaoishi katika umaskini ambao wamekwenda shule. Kuna wengine tumetoka mazingira ya kimaskini, watu kutoka vijijini, wazazi wetu walitupeleka shule na sasa tumekuwa walimu".*

Walimu wawili walitoa ushuhuda binafsi kuhusu udhalilishaji unaotokana na umaskini na madhara yake kwa watoto shuleni.

*"Shule inayo sera ya kuwa na sare sahihi. Wakati mtoto anapokuja shuleni na sare iliyo katika hali mbaya, na ratiba hii ya kila Jumatatu na Alhamisi katika gwaride, wale watoto wenye sare mbaya huamriwa kuja mbele ya*

*gwaride, hivyo kila wakati watoto hao huenda mbele wanapoitwa, na hii huwafanya watoto kudharirika, hivyo kamwe hawapigi hatua mbele, wao hurudi nyuma kwa sababu ya hali yao. Ninao mfano mmoja wa mtoto, kila wakati mimi nilimwita na kamwe hakuja, na siku moja kwa ukali nilimwambia, 'wewe njoo hapa', hivyo alipofika nikagundua kuwa nyuma sare yake ilikuwa imeharibika, hivyo alikuwa na hofu kuja kwangu kwani ni aibu kwake na kusimama mbele ya marafiki zake kwa sababu wao wangemcheka, hivyo kama walimu tuliamua kufanya mchango na kumnunulia sare kwa sababu tulitambua kwamba yeye kamwe hasongi mbele, daima hurudi nyuma".*

Mfano huu ilitolewa na walimu wa Memkwa.

*"Kama mtoto kutoka katika familia maskini amekuwa mtaani kwa miezi kadhaa, ni vigumu yeye kurudi katika muundo na utaratibu wa shule ya msingi. Pia, ni kawaida kwa watoto hawa kukosa baadhi ya vitu vya sare, na watoto wengine huwacheka. udhalilishaji huweza kumfanya mtoto ajihisi vibaya na unaweza haraka kumzuia kuhudhuria shule".*

### 4.6.3. Watoto wenye ulemavu

Kuhusu watoto walemavu, mzazi moja tu aliohojiwa ambaye alikuwa na binti mlemavu. Hata hivyo, wazazi wengine kadhaa na ndugu au majirani wanaishi na watoto ambao ni walemavu.

Ilitaarifiwa kuwa baadhi ya familia huhisi hali ya aibu kwamba mtoto mlemavu ni sehemu ya familia zao. Wazazi waliohojiwa walisema aibu hii inaweza kuwa ni pamoja na *"kumficha"* mtoto nyumbani au kumpeleka kuishi na ndugu kijijini. Watoto wenye ulemavu wanaweza kubaguliwa na wenzao. Hujihisi kwamba wao sio sehemu ya jamii yao na hii husababishwa na matokeo hasi dhidi yao.

Wazazi wanaoishi katika umaskini wanakuwa na wasiwasi kuhusu elimu ya watoto wao wenye ulemavu. Baba mmoja alisema kwamba wazazi wale ambao hupata nafasi katika shule kwa watoto wao wenye ulemavu wao wanapambana kulipia gharama za vifaa vya shule na usafiri. Mama mmoja alisema yeye aliona mhudumu wa basi akimzuia mtoto mlemavu kuingia katika basi na hivyo kumzuia kwenda shule.

Watoto wana ulemavu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ulemavu wa kutembea. Baadhi ya watoto wanao uwezo wa kutumia baiskeli maalumu zitakazowawezesha kufika shuleni, hivyo inawezekana kwa wao kwenda shule kwa

kujitegemea. Hata hivyo, baiskeli hizi zinaweza kuwa ghali na kwa familia maskini sana nje kabisa ya uwezo wao wa kifedha.

Kwa watoto wenye ulemavu zaidi wa kujifunza kama vile mtindio wa ubongo, kwa kawaida wanahitaji vifaa maalum, mbinu mbalimbali za kufundishia na mitaala tofauti, ambavyo ni nadra kupatikana katika shule nyingi za msingi. Bila kujali asili ya ulemavu, watoto wote wenye ulemavu wanahitaji kipaumbele maalum wakati wakiwa shuleni. Hii inaweza kujumuisha walimu kupata mafunzo ya ziada, msaada wa ziada kwa ajili ya walimu darasani, vifaa na mahitaji maalum ya kila mtoto.

Kupitia matatizo yote na maoni yaliyojadiliwa na wazazi, watu kwa ujumla walisema ulemavu haupaswi kuwa sababu ya watoto kutokwenda shule. Watoto wenye ulemavu wanapaswa kupata haki zao za kielimu kwa kutekeleza uwezo wao kama ilivyo kwa watoto wengine. Hata hivyo, kwa familia maskini sana wao watapata changamoto kubwa zaidi ili kuhakikisha watoto wao wenye ulemavu wanaweza kwenda shule.

### 4.6.4. Masomo ya ziada

Serikali iliamua kufuata mfumo wa Elimu Bure Januari 2016, wengi walipata matumaini kuhusu michango mbalimbali na ada ya masomo ya ziada kundolewa, hasa kwa familia maskini sana. Sera hii ilipokelewa kwa shauku na familia nchini kote. Hata hivyo, wadau wote wanahitaji muda wa kuzoea mfumo huu mpya. Hii itajenga fursa kwa walimu, watoto na wazazi kujenga uhusiano mpya kwa kuzingatia uaminifu na kulenga watoto kufanikiwa katika elimu ya msingi. Wakati wa mahojiano, sera hii ilikuwa bado kutekelezwa na michango, pamoja na ada za masomo ya ziada, ilikuwa mojawapo ya hoja nzito zilizoongelewa kuhusu elimu.

Masomo ya ziada yalikuwa moja ya hoja iliyokuwa iliyoongelewa zaidi na wazazi wengi katika utafiti huu, hasa fedha wazazi walizotakiwa kulipa katika miaka ya nyuma. Watoto, wazazi na walimu walionyesha athari chanya na hasi pia madhara ya masomo ya ziada.

Wazazi walikuwa wazi katika majadiliano juu ya ukweli kwamba masomo ya ziada yanaweza kuwa na baadhi ya matokeo chanya kwa elimu ya watoto. Mzazi mmoja alitoa mfano kwamba masomo ya ziada ni muhimu kwa watoto kuhudhuria wakati shule zinapokuwa zimefungwa. Alisema, "*Kwa wale watoto ambao wazazi hawawezi kuwapeleka watoto kwenye masomo ya ziada wakati wa likizo wakati wakifungua shule huonekana kama wanaanza upya".* Mzazi mwingine alisema, *"Masomo ya ziada humsaidia mtoto*

*kukumbuka nini anasoma. Wakati mwalimu akiwafundisha watoto katika masomo ya ziada, masomo hayo husaidia elimu ya watoto kuboreka zaidi, masomo ya ziada yanao mchango mkubwa na msaada kwake ili kuendelea na elimu"*. Mzazi mwingine alisema kwamba pale mtoto anapokuwa amekosa vipindi vya kawaida kwa sababu yoyote, masomo ya ziada yanaweza kumasaidia kuelewa kipindi ambacho amekikosa. Mzazi mmoja alisema, *"Masomo ya ziada ni muhimu, yanaweza kuwaepusha watoto kujiunga na vikundi visivyofaa, huwafanya watoto kuwa na pilika mpaka wakati wa kwenda nyumbani kutoka shule. Hii husaidia watoto kukaa na watoto wengine ambao wanataka kuzingatia na kujifunza, na si kwa kuwa katika makundi mabaya".*

Hata hivyo, wazazi wengi walikuwa wazi katika mawazo yao kuhusu masomo ya ziada walisema masomo ya ziada hayamsaidii mtoto na wao huona hakuna tofauti wakati wa mitihani. Wanashindwa kuelewa ni kwa nini masomo ya ziada hayawezi kufundishwa wakati wa vipindi vya kawaida vya darasani. Wazazi waliruidia kusema kwamba mara gharama za masomo hulemaza mahitaji ya familia zao, hasa wakati wao wanapokuwa na watoto kadhaa kuhudhuria shule.

Habari za masomo ya ziada ambayo walimu walifundisha, walimu wachache walikuwa tayari kuzungumzia hili moja kwa moja. Mwalimu mmoja alisema, *"Siwezi kusema chochote kuhusu masomo ya ziada, haya ni maamuzi kati ya kamati ya shule na wazazi"*. Mwalimu mwingine aliainisha kuwa masomo ya ziada *"ni makubaliano"* kati ya wazazi na kamati za shule. Kiongozi wa serikali ya mtaa ambaye yupo katika kamati ya shule, alisema ili kuboresha kiwango cha elimu ya watoto waliweka *“masaa ya* (masomo) ya *ziada*” kwa makubaliano na wazazi.

Kwa kiasi kikubwa maoni ya watoto inawezekakana yalikuwa muhimu zaidi yakifafanua kuhusu masomo ya ziada. Wao waliyapa thamani masomo ya ziada, lakini kwa sababu baadhi ya watoto walikuwa wakitengwa na masomo hayo hivyo waliona ni kama ubaguzi kwa watoto wanaoishi katika umaskini ulikithiri.

Watoto walisema kwamba wao walihudhuria mara kwa mara vipindi vya darasani vilivyofundishwa katika muda wa masomo ya ziada, mambo ambayo yalitolewa katika maswali ya mitihani, hii ina maana kwamba wale watoto ambao hawakuhudhuria masomo ya ziada wangeshindwa katika mitihani. Mtoto akasema,

*"Masomo ya ziada ni kweli yanasaidia, lakini baadhi ya watoto wanaweza kulipa na baadhi hawawezi kulipa,*

*hivyo kwa wale ambao hawawezi hawaruhusiwi kuhudhuria masomo ya ziada, hivyo katika mtihani wao wanashindwa wakati wazazi wao watawategemea katika maisha yao ya baadaye"*.

Watoto waliulizwa wanajisikiaje kuhusu watoto wale ambao hawahudhurii masomo ya ziada? Mtoto wa mwanzo akaendelea, *"Najisikia vibaya kwa sababu baadhi ya watoto ambao hawaji katika masomo ya ziada ni marafiki zetu. Mimi ninakuwa na fedha za kutosha kujilipia mwenyewe, siwezi kuwalipia na marafiki zangu. Hivyo baada ya masomo ya ziada sisi hujaribu kutafuta muda wa kuwaelezea kile tulichojifunza katika masomo ya ziada, na kumsisitiza rafiki awe makini juu ya kile nilichomwambia".*

Kilichojitokeza sana kutoka kwa watoto ni kwamba masomo ya ziada huwanyanyasa watoto maskini. Mtoto mmoja akasema, *"Wakati watoto ambao hawakwenda kwenye masomo ya ziada wameshindwa kwenye mitihani walimu wanasema maneno mabaya juu yao. Wanasema, 'Angalia, wale ndio ambao hawakulipa', hivyo watoto hao kujisikia vibaya sana na kuumia".* Mtoto mwingine alisema, *"Mtoto hujisikia vibaya sana kuona marafiki zake wamefeli katika mitihani kwa sababu hawakwenda tuisheni, lakini katika madarasa ya kawaida ni wazuri sana katika masomo yao ya kawaida, walishindwa kwa sababu ya hali za wazazi wao ndio maana hawawezi kulipa. Mimi pendekezo langu kwa mwalimu ni kutombagua mtoto yeyote ambaye hana fedha leo, kwa sababu kesho atapata".*

Kuhusu athari kwa watoto wale ambao hawaruhusiwi kuingia tuisheni mtoto mwingine aliendelea kusema, *"Tunajisikia vibaya sana kwa sababu sisi wote tunataka kufanikiwa, na kwa nini wengine wanashindwa".* Maneno ya mtoto huyu yalijazia vizuri kile wanachoamini lazima kitokee ili kuzuia tabia hii ya ubaguzi,

*"Tunajisikia vibaya sana kwa sababu tuna lengo moja la kufanikiwa, tunaona si haki kwa baadhi yetu kufeli, tunaomba walimu wafanye jambo sahihi, kwa wote, hata kwa wale ambao hawana uwezo wa kulipa".*

### 4.6.5. Uji

Hitimisho lilifanywa kuhusu zoezi la utoaji uji kwa watoto mashuleni. Huu ni ubaguzi dhidi ya watoto maskini. Baba mmoja alisema, “baadhi ya wazazi wanao uwezo wa kuwapa watoto wao fedha za kununulia uji, wakati watoto maskini hawana fedha za kununulia uji. Huu ni ubaguzi dhidi ya watoto maskini”. Ni shule chache tu zinzzotoa uji bure. Kwa familia zilizo katika hali ya umaskini uliokithiri kulipia uji kila siku, kwao ni gharama kubwa.

### 4.6.6. Kila kitu kuhusu elimu ni fedha

Utafiti wa hivi karibuni uliotolewa na Twaweza Februari 2016 ulionyesha kuwa 80% ya watu walikubaliana na kauli ifuatayo: *"Walimu wengi wanaonekana kama hawaipendi taaluma yao, lakini wako pale kwa ajili ya kupata fedha tu".* Hii inatia shaka kitakwimu, ni moja ya michango ya wazazi katika utafiti huu. Mara kwa mara wazazi waliongelea kuhusu walimu kupewa *"motisha ya fedha".*

Kama inavyoonekana katika kifungu kinachosema “Kazi na Kipato”. Kipato cha familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri kiko chini sana tena kinachoyumba, kwa hiyo, kulipia elimu ambayo inatolewa na serikali 'bure' inaleta hofu kubwa kati ya familia na wadau wanaotoa elimu. *"Usemi wa elimu ya bure kwa sasa. Hakuna huduma ya bure. Huu ni msemo tu unaosemwa na watu, watu wanasema tu lakini hawana uzoefu”.* Alisema baba mmoja.

Kama ilivyoonyeshwa, upo mvutano mkali kati ya wazazi wengi maskini na walimu na hali ya kutokuwepo na ushirikiano wa karibu. Mzizi huu huonekana tu kutokana na fedha. Wakati wa mradi, watafiti walisikia hadithi nyingi, baadhi za kushangaza, namna walimu wanavyojaribu kutafuta fedha kutoka kwa watoto na wazazi wao. Mama mmoja akasema,

> *"Ninapokuwa na pesa nawaacha waende shule lakini kama sina wanakaa tu nyumbani. Leo huyu anaenda mwingine anakaa nyumbani, siku inayofuata mmoja anakwenda mwingine anakaa nyumbani”.*

Hii ilikuwa ni kawaida kabisa kati ya familia maskini sana. Mama mwingine alisema, *"Hivi sasa wanahitaji nilipe fedha kwa ajili ya mitihani lakini nilikuwa tayari nimeshalipa, hawaniamini”*.

Mzazi mmoja alisema katika shule ya mwanae, walimu hawana mipaka katika kutafuta fedha kutoka kwa watoto. Alitutaarifu, *"Mwalimu kufanya ukaguzi mkubwa kusaka fedha. Huangalia katika mifuko yao na wasipopata chochote huwakagua hadi katika soksi zao".* Mzazi mmoja alituambia kwamba siku nyingine mtoto wake huenda shule bila fedha kwa ajili ya michango. Mwalimu huwaruhusu watoto hawa kuingia darasani, lakini kama adhabu anawaambia kuugeuzia uso ukuta nyuma ya darasa na si kuangalia ubaoni ambapo anafundisha somo, akiwazuia watoto hao kujifunza. Mtazamo wa mzazi huyu ni kwamba katika mazingira kama hayo ni bora kupeleka mtoto wake nyumbani badala ya kuwadhalilisha watoto kwa kuwakatalia nafasi ya kujifunza.

Baba alieleza kuhusu kuchanganyikiwa kwake katika kujaribu kushirikiana na shule ambapo mtoto wake anahudhuria. Alisema baadhi ya wazazi hupewa muda wa

kuongea na husikilizwa, lakini baadhi hupuuzwa. Aliwaeleza walimu kuhusu maisha magumu ya familia yake na kuuliza kuhusu uwezekano wa kupunguziwa michango inayotakiwa kwa watoto wake, lakini walimu hawakuwa tayari kumsikiliza. Mwalimu mmoja alimwambia, *"Kama wewe huna fedha mwache mtoto wako akae nyumbani".* Alisema, *"Mwalimu anapokuambia kumwacha mtoto wako nyumbani hauna kingine cha kumwambia."*

Wazazi walisema tena na tena kwamba wakati walimu wako makini kutafuta njia za kupata fedha ya (masomo, uji, ada ya usalama, n.k) watoto wataendelea kufeli katika elimu yao ya msingi.

Kuhusu michango yote mbalimbali iliyokuwa inahitajiwa, hali ya kutofahamu matumizi ya michango ni suala lililokatisha tamaa na pengine kuwafanya wazazi waamini kwamba walimu huiweka hiyo pesa kwa ajili yao wenyewe. Wazazi walifadhaika kuendelea kutoa michango kwa ajili ya dawati kila mwaka mpya wa shule wakati watoto wakiendelea kukalia sakafu. Wazazi wanachukia wao kulipia maji wakati vyoo hubaki katika hali isiyo salama na isiyokuwa ya usafi. Wazazi wanakereheka kuona kwamba wanalazimika kulipa ada ya masomo ya ziada wakiogopa kwamba watoto watashindwa kuhitimu shule ya msingi wasipolipa. Mzazi mmoja alikuwa wazi sana na alisema, *“Kama michango inapaswa kulipwa kwa sababu maalum wazazi wanapaswa kujua hasa fedha hiyo imetumika vipi”.*

Vilevile walimu walipewa nafasi ya kujibu maswali kuhusu michango shuleni. Walimu walisema kwamba fedha zinazotolewa na serikali shuleni hazitoshi, hivyo wazazi waliombwa kuchangia.

Walimu kadhaa walisema michango ya wazazi waliyotakiwa kulipa ni vigumu kwa baadhi ya familia kupata, na hii ina athari hasi kwa elimu ya watoto. Walimu walisema,

*"Kwa sababu serikali haitoi msaada wa kutosha (shuleni) kulipia maji, umeme na ulinzi, walimu walilazimika kuwaambia wazazi kuchangia. Kama mzazi hana anamwambia mtoto, 'Kaa nyumbani' na hivyo mtoto hukosa masomo".*

Mwalimu mwingine alisema, *"Itakuwa vizuri kama serikali inaweza kuruhusu wazazi kuchangia fedha, hasa katika maandalizi ya mitihani kwa sababu fedha kutoka serikalini hazitoshi".*

Hata hivyo baadhi ya walimu walisema si wazazi wanaopaswa kulipia elimu ya watoto wao na rasilimali zinazohitajika shuleni, bali ni serikali.

Ingawa wazazi walikuwa hawafurahishwi na mbinu za walimu katika kujipatia kipato cha ziada, karibu wazazi wote

walikubaliana na wazo kwamba mishahara ya walimu inapaswa iongezwe.

Baba mmoja alisema, "*Katika sekta ya elimu endapo posho za walimu zingekuwa nzuri ili kuwawezesha kukidhi mahitaji yao, nadhani kwamba elimu ya watoto ingeweza kuongezeka kwa sababu walimu hawataweza kuwa na wasiwasi sana wa kazi zao kwa sababu fedha wanayopewa ni nzuri*". Mzazi mwingine alisema.

*"Wao mara nyingi hufanya kazi shule zilizo mbali na mahali wanapoishi, hawapati msaada wowote wa usafiri, na hulazimika kukodi nyumba karibu na shule ambayo inaweza kuwa ghali. Serikali haiwajali".*

Wazazi walihojiwa, *"Endapo utapata nafasi ya kuzungumza na waziri wa elimu ungemwambia nini?".* Wazazi wote walisema kumwomba kukoma kwa michango yote, iwe ya kila mwaka, kila mwezi, kila wiki au kila siku. Walisema kukomeshwa kwa kudumu kwa michango kutawafanya watoto wasiogope kwenda shule na hawatakuwa na uoga wa kuadhibiwa na kurudishwa nyumbani.

### 4.6.7. Kushuka kwa elimu

Ingawa lengo la kwanza la utafiti halikuwa katika ubora wa elimu, wazazi waliombwa kutoa maoni yao juu ya hoja tatu maalum: Kwa nini baadhi ya watoto humaliza shule ya msingi wakiwa hawajui jinsi ya kusoma na kuandika; Ni changamoto zipi zinachangia mwanafunzi kushindwa kuhitimu shule ya msingi; Ni changamoto zipi zinachangia zaidi kupungua kwa utendaji kielimu. Majibu yaliyotolewa yanaleta ufahamu katika baadhi ya changamoto ambazo watoto maskini hukumbana nazo katika kupata na kumaliza elimu ya shule ya msingi.

Katika ripoti hii, idadi ya maeneo yamekuwa yakitambulishwa kama ukweli mkubwa kuhusu kwa nini baadhi ya watoto hushindwa kumaliza elimu yao ya msingi, ikiwa ni pamoja na mazingira ambayo wanaishi au kupita kwenda shule, masuala ya afya, ukosefu wa rasilimali fedha, nk Hata hivyo wazazi pia walikuwa wakweli kwa kusema kwamba baadhi ya watoto ni *"watovu wa nidhamu"* na/au ni *"wavivu"* linapokuja suala la kwenda shule. Baba mmoja alisema, *"Malezi ya mtoto kutegemea mapenzi yake katika elimu yanaweza kuwa na athari kubwa katika kumaliza kwake elimu ya msingi".* Aliendelea kusema,

"Unakuta mpaka mtoto wako alimaliza darasa la saba yeye hajui kuandika au kusoma, hivyo kuanza kuwalaumu walimu kwamba hawafundishi, wakati ni tabia ya mtoto wako mwenyewe".

Watoto kuwa watoro au kutokwenda shule ilionekana kama moja ya sababu kubwa kwa nini watoto hushindwa kujifunza

kusoma na kuandika kabla ya kumaliza shule ya msingi. Ingawa utoro haukuwa sababu pekee ya watoto kuwa wavivu au wasiotii, kuna sababu nyingi zinazochangia kupelekea hili ikiwa pamoja na umaskini katika familia, kushika majukumu ya kiutu uzima, n.k. Pengine watoto wenzao pia huwafanya kuwa watoro kwa kuwashawishi kwenda kutembelea pwani, mitaani au vinginevyo hadi muda wa shule unapokwisha na kisha hurejea nyumbani.

Ilikuwa ni vigumu kwa baadhi ya wazazi kuelewa ni kwa nini watoto wao wanakuwa watoro. Wazazi wengine walisema kuhusu kuwaadhibu watoto wao kwa kutokwenda shule. Jambo la wazi ni kwamba sababu zipo na hasa kwa watoto kutoka familia maskini sana sababu hizo inaweza kuwa ngumu na wakati mwingine kutoeleweka. Mama mmoja alisema,

*"Walimu huwaadhibu wanafunzi ambao wameshindwa kulipa michango mpaka baadhi yao wanakataa kwenda shule"*

Kwa wazazi ni dhahiri kwamba mtoto ambaye haudhurii shule haupo uwezekano wa kusoma na kufuzu elimu ya msingi.

Walimu walikuwa na maoni ya wazi kuhusu kushuka kwa elimu. Mwalimu mmoja tu alikanusha kuhusiana na kushuka kwa elimu. Sababu za kushuka kwa elimu ilikuwa ni pamoja na; mfumo wa elimu ikiwa ni pamoja na mitaala, ukosefu wa vifaa vya kufundishia kama vile vitabu vya kiada, madawati ya kutosha, na msongamano wa wanafunzi madarasani jambo ambalo lilisababisha baadhi ya watoto kukaa juu ya sakafu. Viongozi wa serikali za mitaa na wajumbe wa kamati za shule pia walikuwa na wasiwasi sana kuhusu idadi ya watoto bila madawati. Watoto wote waliohojiwa walizungumzia kuhusu kuchanganyikiwa kwao kutokuwa na vitabu vya kutosha na madawati. Pia wazazi walitambua tatizo la msongamano madarasani na haja ya shule za msingi zaidi, madawati na vifaa vingine ili kuondokana na hali hii.

Mara nyingi walimu waliripoti kufundisha watoto 100 au zaidi katika darasa. Mwalimu mmoja alisema, *"Watoto hawawezi kuelewa vizuri ikilinganishwa na darasa lenye wanafunzi 45".* Mwalimu mwingine alisema wakati watoto wamekaa sakafuni na hawana vitabu vya kiada vya kutosha, elimu kamwe haitaboreshwa. Mwalimu Mkuu mmoja aliripoti kuwa kuna walimu wa kutosha katika shule yake kwa idadi ya madarasa aliyokuwa nayo, lakini katika baadhi ya madarasa yao walikuwa na watoto 200. Mwalimu mwingine alisema,

*"Kwa idadi hii kubwa ya wanafunzi nafanya kile ninachoweza".*

Ufumbuzi ambao shule ilitumia ili kuondokana na tatizo la msongamano wa wanafunzi madarasani ni kuwaambia

baadhi ya watoto waje shuleni asubuhi, 02:00-6:00, na watoto wengine kuja mchana 06:00-10:00. Hata hivyo, mwalimu mmoja alisema hii ilileta changamoto ya kufundisha masomo mengi katika kipindi cha saa nne.

Mwalimu anayeishi mbali na shule hukabiliwa na changamoto ya safari ndefu nyakati za asubuhi na jioni. Hawana kabisa muda wa maandalizi kwa ajili ya masomo kabla ya watoto kufika.

Mwalimu mmoja aliukosoa mfumo wa sasa wa elimu kwa sababu watoto humaliza shule bila kujua kusoma na kuandika. Alisema kuwa katika siku za nyuma kulikuwa na msisitizo mkubwa juu ya msingi wa kuhesabu na kusoma, lakini sasa mafunzo ya masomo yanapelekwa haraka haraka katika masomo ambayo watoto hawawezi kuelewa. Mtaala mmoja wa kitaifa ulipendekezwa na walimu wengi pamoja na uboreshaji wa vitabu vya kiada vinavyotumiwa kwa ajili ya kufundishia.

Baadhi ya walimu walikosoa sana mtindo wa ufundishaji wa walimu wengine, kama vile kufundisha masomo *"waliyopenda"* kutoka katika vitabu vya kiada na sio kulingana na mtaala. Hii inaweza kuleta tatizo wakati wa mitihani kama watoto hawajafundishwa mtaala sahihi. Walimu pia waliripoti juu ya kuwepo kwa vitabu kadhaa kwa somo moja, jambo ambalo linaweza pia kuwachanganya watoto kama watafundishwa kutoka katika vitabu tofauti. Mwalimu mmoja alisema kwamba alikuwa ameona watoto wakitumia vyombo vya habari vya kijamii na kutafuta katika mitandao kupata majibu kwa ajili ya kazi walizopewa darasani, badala ya kutafuta majibu katika vitabu vya kiada. Mwalimu mwingine alisema, *"Hakuna mjadala kati ya wale waliotengeneza mtaala wa sasa na walimu".* Mfano wa hili ulitolewa na mwalimu ambaye alisema kuwa sasa somo la Tehama lilianzishwa katika baadhi ya shule, lakini wao hawakuwa na kompyuta na walimu hawakupewa mafunzo ya jinsi ya kufundisha somo hilo.

Sababu nyingine iliyotolewa kuhusiana na kushuka kwa elimu kunakosababishwa na walimu ni mfumo wa mitihani wa sasa ambao hauwalazimu watoto kufikiri kwa kina. Maswali ya kuchagua katika mitihani kunaweza kusababisha baadhi ya watoto kupita kwa kubahatisha. Mfumo huu una maana kwamba watoto upo *"uwezekano"* kwamba wanaweza kufanikiwa katika masomo ambayo wanayo maarifa kidogo sana.

Mwalimu mmoja alisema baadhi ya wanafunzi wana uwezo mkubwa wa akili, na baadhi wana uwezo mdogo, hivyo baadhi ya walimu huangalia darasani wale wenye uwezo wa juu na kuweka juhudi zao katika kufundisha watoto hawa.

Kushuka kwa elimu, kwa mujibu wa walimu lilikuwa pia jukumu lao. Mshahara wa mwalimu ulionekana tena kama

usiojitosheleza, jambo ambalo "*Hufanya walimu wawepo pale kimwili lakini kiakili wako nje*". Walimu wanatakiwa kujua umuhimu wa elimu ili kuhakikisha kuwa wanafundisha vizuri. Moja ya changamoto zilizoripotiwa na mwalimu mkuu ilikuwa kuhusu wafanyakazi wake. *“Walimu wana historia tofauti, hivyo ukimweleza mwalimu 'usifanye hivyo', lakini asili ya utu wake inamfanya anachotaka kufanya yeye*".

Mtoto anapokuwa hajafika shule kwa miezi mitatu, jina lake huondolewa kutoka kwa rejista. Memkwa ni darasa la kujitolea kwa ajili ya watoto ambao wamekuwa watoro kutoka shule kwa miezi au miaka mingi. watoto katika darasa inaweza kuwa wa umri tofauti. Mwalimu wa Memkwa aliripoti kwamba yeye hapati bajeti kwa ajili ya vifaa anavyohitaji kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la Memkwa. Kwa sababu ya tofauti ya umri na idadii ya watoto, mara nyingi hana budi kupita madarasa mengine na kuomba kuazima vitabu kutoka kwa walimu wengine.

Ili kukabiliana na kushuka kwa elimu wazazi walizungumza kuhusu umuhimu wa ukaguzi, ikiwa ni ukaguzi wa ndani shuleni, au ufanywe na wakaguzi wa serikali. Wazazi wangependa kuona Waziri wa Elimu akitoa maelekezo kuhusu ukaguzi wa shule. Wazazi walisema sera nyingi nzuri na maneno mazuri yamezungumziwa kuhusu elimu ya msingi lakini hakukuwa na ufuatiliaji au zaidi yamekuwa maneno maneno tu.

### 4.6.8. Urafiki

Watoto wote waliohojiwa walisema kuwa wana marafiki shuleni. Walitoa mifano mingi ya namna ambavyo wanashirikiana na kila mmoja: kukaa pamoja katika vikundi na kusoma pamoja; mmoja hufanya makosa, husaidina na kusahihishana; kusaidiana kama kuna kitu kilisemwa na mwalimu na hakikueleweka; endapo mtu alikosa kufanya kazi kwa sababu yoyote, wengine kumsaidia kushika haraka; wakisaidiana na kwenda na kumuona mwalimu pamoja; hutiana moyo na kuandamana pamoja kwenda na kutoka shule; na kuzungumza na kufurahi kwa nyakati tofauti.

Kushirikishana matatizo yao na kupeana kushauriana ni msaada mkubwa wanaopeana. Mtoto mmoja alitoa mfano kwamba wakati yeye anaona wazazi wake wakizozana, huenda kujadili na marafiki zake, mtoto mwingine alizungumzia jinsi anavyopigwa nyumbani na wazazi wake hivyo marafiki zake humshauri tabia nzuri za kufuata.

Mtoto mmoja alihitimisha yote vizuri sana jinsi ambavyo watoto husaidiana katika masomo yao,

> *"Nina marafiki wengi, tunapenda kujifunza pamoja,*
> *nikiwa na tatizo kwenye masomo nakwenda kuomba*

*msaada kwa marafiki zangu. Kile ninachokijua nawashirikisha na watu wengine, tunajadili na kutafuta majibu pamoja".*

Kuwa na marafiki shuleni ni msaada mkubwa na sehemu muhimu kwa maendeleo ya kijamii kwa watoto. Hata hivyo, urafiki unakuwa na changamoto wakati mwingine, ikiwa ni pamoja na: kuudhiana, kutoelewana, kugombana, kupigana, na kuwaibia wanafunzi wengine; kujifunza tabia mbaya na kuhamasishana kutega vipindi vya darasani; kuwaambia wazazi wa marafiki zao siri zao na tabia zao mbaya, mambo ambayo huvunja urafiki. Baadhi ya watoto hawako tayari na hata hukataa kuwasaidia wengine katika masomo yao. Mfano mmoja uliotolewa ulikuwa kwamba watoto wakubwa hawawasaidii wadogo zao hata kama hao wadogo zao wanaelewa kazi za shule. Pia baadhi ya watoto walisema walipewa taarifa zisizo sahihi na watoto wengine na kuwafanya kushindwa katika kazi za darasani au mitihani.

Mtoto mwingine alizungumzia uonevu shuleni, akasema kwamba makundi ya watoto yapo katika shule. Alisema kuna kundi la watoto wabaya katika shule ambao humpiga na kuiba fedha zake, lakini wakiwaelezea walimu wao, huwahofia watoto hao.

### 4.6.9. Usalama/Adhabu

Moja ya maswali yaliyoulizwa wakati wa utafiti lilikuwa kama wazazi wanafikiria kuwa shule ni mahali salama kwa watoto wao. Maoni ya wazazi juu ya suala hili yalikuwa mchanganyiko kabisa, lakini muhimu sana. Baadhi ya wazazi walieleza wasiwasi wao kuhusu mazingira ya shule, hasa vyoo kutokuwa katika hali safi na wasiwasi wao kuhusu magonjwa ya kuambukiza kuwaandama watoto. Mzazi mmoja alisema kuwa vyoo lazima kusafishwa na watoto lakini kukaguliwa na walimu ili kuhakikisha usafi. Wazazi wengine walizungumzia usalama katika suala la Shule kuwa mahali inapotolewa elimu nzuri na *"maadili"* mema kwa watoto, ambayo yana faida kwao, familia zao na jamii kwa ujumla. Pia wazazi waliongelea imani waliyonayo kwa walimu, walisema walimu ni watu ambao ndio wa kwanza kutoa usalama kwa watoto shuleni.

Watoto kutoka shule moja waliohojiwa wana uhusiano mzuri sana na mwalimu mkuu. Walisema kama mwalimu ni mkali na hawaelewi somo, wanajua wanaweza kwenda kwa mwalimu mkuu na kumdokezea, kama mkuu, atazungumza na mwalimu husika. Kwa watoto kuwa na uwezo wa kumwamini mwalimu wao mkuu ilikuwa ni faraja kubwa.

Wasiwasi mkubwa walionao watoto wakati wa kusoma ni mwitikio wa baadhi ya walimu. Karibu watoto wote waliohojiwa walisema kuwa baadhi ya walimu ni wakali sana, jambo linalowafanya watoto kusita kuwasogelea.

Watoto walisema kuwa *"wanaogopa"* kuwakaribia baadhi ya walimu na kuomba msaada kama hawakuelewa swali. Mtoto mmoja alisema yeye huanza *"kutetemeka"* akimwona mwalimu fulani. Watoto walisema hupata wasiwasi wakiona walimu wamebeba fimbo darasani, mtoto mmoja alisema yeye anajua majibu ya maswali lakini husahau pale anapomwona mwalimu amebeba fimbo.

Athari hizi zimesababishwa na hofu ya kupigwa. Watoto walirudia kusema, kama wakifanya makosa walimu huwapiga. Watoto walisema kupigwa hakuwafanyi waache kufanya makosa katika mwendo kazi, bali huwafanya kuwa na hofu. Kwa watoto ambao wanahofia walimu walisema hawakuweza kujifunza vizuri katika masomo hayo.

Hofu ya watoto dhidi ya walimu pia iliongezeka kwa tatizo la kwenda shule bila fedha kwa ajili ya uji, masomo au ada ya mitihani ya kila wiki. Watoto walisema kama hawana fedha, hurudishwa nyumbani, mara nyingi wanajua kuwa wazazi wao hawana fedha za kuwapa. Siku iliyofuata wakiwaomba wazazi wao pesa, wanaambiwa hakuna. Watoto walisema huenda shule siku hiyo wakijua kuwa watapigwa na mwalimu ambaye aliwarudisha nyumbani siku iliyopita.

Kwa watoto wanaokuja shule bila michango ya masomo, wametoa taarifa kwamba walimu huwapekua mifuko yao kwa ajili ya kutafuta fedha. Watoto hao ambao wanasema hawana fedh hutengwa katika kundi, wakati wale ambao wana fedha wanaruhusiwa kuingia darasani. Wale waliotengwa hupekuliwa, na endapo watapatikana na fedha huadhibiwa. Kitendo hiki cha kupekuliwa mbele ya wenzao ni udhalilishaji mbaya.

Ukali wa baadhi ya walimu, kama ilivyoripotiwa na watoto, ilikuwa pia sehemu ya maoni ya walimu. Kama mtoto anakaripiwa na mwalimu darasani kwa kutoelewa, mtoto huyo kamwe hatarudia tena kuuliza maswali. Hii inaweza kusababisha mtoto si kutoelewa tu bali pia hatimaye kuacha shule.

# 5. MAPENDEKEZO



**5.1.** Serikali kuu inapaswa kuzipatia shule walimu, vifaa na nyenzo muhimu kwa ajili ya kuwakaribisha na kuwaelimisha watoto wote, wakiwemo watoto walemavu kwa kuwapatia elimu yenye kiwango katika shule za msingi. Walimu wanapaswa kupata mafunzo endelevu na mishahara yenye kukidhi gharama za maisha.

**5.2.** Mudana mahali panapowezekana, watoto waishi maeneo yasiyo mbali na shule za msingi. Watoto hawasumbuliwi kuingia kwenye mabasi wakati wa kwenda na kurudi shule.

**5.3.** Serikali ya mtaa kwa kushirikiana na wazazi pamoja na jamii kwa ujumla wanapaswa kuchukua hatua muhimu za kuwatengenezea watoto mazingira salama, ikiwemo mpango madhubuti wa kuzuia watoto kujiunga na makundi ya uhalifu na kuwakataza wamiliki wa mabanda ya kuonyesha luninga na michezo kuwaruhusu watoto kuingia muda wa kwenda shule.

**5.4.** Kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaandikishwa, wazazi, wajumbe wa nyumba kumi na serikali za mtaa wanapaswa kuwa karibu sana na kushirikiana na shule za msingi.

**5.5.** Kila kitongoji kiwe na sehemu ambayo wazazi na watoto wanaweza wakapata ushauri na msaada katika huduma za elimu.

**5.6.** Wazazi wanapaswa kuwapatia watoto wao sare za shule, begi, viatu na kalamu. Wanapaswa kuwahamasisha watoto wao kusoma na kuwasikiliza hofu zao. Wazazi wawape watoto kazi za nyumbani zilizo ndani ya uwezo wao na zisizoingiliana na kazi zao za shule ya msingi.

**5.7.** Washikadau wote wa elimu lazima wakubaliane na sera ya elimu bure kuhusiana na michango ya fedha.

**5.8.** Shule zinatakiwa kuhamasisha urafiki kati ya watoto ili kufikia malengo yao.

**5.9.** Kila mwanafunzi wa shule ya msingi anapaswa kuwa na fulsa ya kumona muuguzi shuleni, vitendea kazi na vifaa. Muuguzi anatakiwa kushirikiana na wazazi na kuwasaidia, kwa ushauri na matibabu ya watoto.

**5.10.** Adhabu za vitendo kwa watoto lazima zitokomezwe. Wazazi na walimu wanapaswa kukubaliana ni aina gani ya adhabu zisizoumiza mwili zitumike.

**5.11.** Kuwepo na mfumo wazi wa mawasiliano kati ya walimu na wazazi. Mawasiliano yanaweza kuwa kwa njia ya mikutano, simu, barua au kutembeleana.

**5.12.** Kujenga uaminifu na kuboresha mahusiano, washikadau wote wa elimu wanapaswa kuendeleza kutambua kuheshimiana kuhusu hali za wengine.

**5.13.** Kila shule inapaswa kuwa na mfanyakazi wa kuifikia jamii ambaye jukumu lake ni kutengeneza mahusiano kati ya walimu na wazazi na kuhakikisha uwepo wa mawasiliano ya mara kwa mara haswa kwa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri.

**5.14.** Mikutano ya shule iandaliwe na walimu wakuu na wawakilishi wa wazazi. Mikutano iwe ni sehemu ya wazazi na walimu kubadilishana uzoefu na changamoto wanazokutana nazo na kulenga zaidi maendeleo ya elimu ya watoto. Ni muhimu kwamba mawazo ya wazazi yasikilizwe.

**5.15.** Kama wazazi wana malalamiko kunatakiwa kuwe na hatua wazi za kufuata na wahakikishiwe kuwa hakutakuwa na matokeo mengine kama watalalamika.

# 6. HITIMISHO



Katika utafiti, wazazi, walimu na watoto walisema,*"Elimu ni ufunguo wa maisha"*. Kwa watoto wanaotoka katika familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri, ili kuupata huu *'ufunguo'* hali fulani lazima zifikiwe. Hata hivyo ili mapendekezo ya utafiti yaweze kutekelezwa siyo tu jukumu la shule na walimu, bali pia watoto na marafiki zao, wazazi na wanafamilia wengine, majirani, jamii katika mapana yake, serikali za mitaa na serikali kuu Hitimisho hili linaangalia kile tulichojifunza kupitia mradi huu wa utafiti na kutoa msingi wa mapendekezo.

Utafiti umeonyesha jinsi ilivyokuwa muhimu kufanya kazi kwa kushirikiana na watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Ushiriki wao uliongeza thamani kwa sababu ya ujuzi wa kipekee waliouleta kutokana na uzoefu wao wa maisha, hasa katika jambo hili linaloathiri maisha yao na jamii zao kwa upana.

Kuhakikisha kwamba watu walio na uzoefu wa maisha katika umaskini uliokithiri waliweza kushiriki kikamilifu kama watafiti halisi mazingira sahihi yalitakiwa yapatikane ikiwa pamoja na: mabadiliko katika nyakati za kazi; kuhakikisha watu wenye ujuzi mdogo kuandika wanaweza kushiriki katika ngazi moja: kutoa msaada kwa ajili ya kushiriki kwao bila ya athari hasa katika familia zao: kusikiliza kwa makini na kuyajenga mawazo yao ambayo si mara zote yalikuwa yanaeleweka mara moja.

Katika kila hatua katika utafiti ilikuwa mara nyingi ni muhimu kujaribu njia bora ya kusonga mbele. Kwa mfano, asubuhi ya kwanza tulifanya kazi juu ya mapendekezo, ilikuwa changamoto kwa watu wenye uzoefu wa umaskini uliokithiri kwa kutoa mapendekezo kutoka kwenye matokeo ya utafiti na sio kutokana na uzoefu wao wa maisha. Ilichukua muda na maelezo zaidi hadi kundi kupata njia ya kuelewa kazi na kuendelea. Siku zilizofuata kazi ilieleweka na iliendelea vizuri tena na ufahamu zaidi.

Moja ya faida muhimu za kuwa na watu wanaoishi katika umaskini ulikithiri katika utafiti ilikuwa uhusianao wao na wahojiwa wakati wa mahojiano. Mtafiti mwenye uzoefu katika maisha ya umaskini uliokithiri alimhoji mama mwenye watoto wanne, ambaye alizungumzia kwa uwazi changamoto zote zinazomkabili tokea mumewe alipofariki. Mtafiti aliweza kuelewa na kupata ufahamu wa hali nzima wakati huo huo akiendelea na jukumu lake la kumhoji katika mihimili ya utafiti bila kupoteza jukumu lake kama mtafiti.

Timu ya Utafiti ilipanua uelewa wao wa umaskini uliokithiri kuwa ni pamoja na kunyimwa haki za msingi, ubaguzi na udhalilishaji, si tu ukosefu wa fedha.

Umaskini uliokithiri hutengemeza kuyumba na kutokuwa na uhakika katika maisha. *"Kinachonipa mashaka ni pale inapoanza siku mpya, nitaihudumiaje familia yangu leo?"*

Kwa familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri matatizo yanapotokea yanakuja ghafla na wanakuwa hawana rasilimali kukabiliana na matatizo. "*Wakati tatizo linapotokea sina muda wa kutatua tatizo, nalitatua kadiri linavyojitokeza".* Wakiwa katika maisha yao ya siku kwa siku, watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri hawawezi kutengeneza rasilimali ambazo wanaweza kuzigeukia wakati wa dharura. Badala yake hutengeneza mikakati ya muda mfupi kutatua matatizo yanayowakabili.

Ukosefu wa mara kwa mara wa fedha na kutokuwa na uhakika huleta wasiwasi na mvutano katika maisha ya familia maskini sana. Fedha zinahitajika kwa ajili ya mahitaji ya misingi katika maisha, malazi, chakula, maji, afya na elimu. Hata hivyo, maisha si tu kuhusu mahitaji ya msingi na kuishi, fedha zinahitajika kuwa sehemu ya familia mchanganuo na jamii na kufurahia shughuli za kitamaduni na kijamii. Wakati wazazi wanapotakiwa kufanya maamuzi magumu juu ya jinsi ya kutumia fedha kidogo wakati mwingine wanaonekana kwamba hawawajibiki. Mgeni anapowatembelea ni kawaida kumpatia cho chote hata kama ni kikombe cha chai. Hiyo inamaana kwamba pesa iliyokuwa imehifadhiwa kumnunulia mtoto kalamu imetumika kumnunulia mgeni sukari. Watoto wanapokwenda shule bila kalamu huambiwa wazazi wao ni wavivu bila kuelewa mazingira ya nyumbani kwao. *“Wazazi wenu ni wavivu, hawana mikono na miguu ya kufanya kazi”.*

Utafiti uligundua kuwepo kwa chuki zisizo na msingi dhidi ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Mhojiwa mmoja alisema baadhi ya watu maskini "*kujifanya*" kuwa maskini ili wasilipe michango. Mhojiwa mwingine alisema wazazi, "(...) *hawawezi kuchangia kwa watoto wao lakini wanaweza kutekeleza mambo yao wenyewe*". Familia maskini sana mara nyingi wanatuhumiwa, kulaumiwa na kuwajibika kwa ajili ya maisha yao. Wao wanaukumiwa kwa maamuzi yao bila kujua sababu na changamoto zinazoendesha chaguzi zao.

Wasiwasi mkubwa unaowakabili watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri ni kuwa na makazi. Kulegelega kwa kutokuwa na makazi kunatokana na vyanzo vingi, kama vile kutakiwa kuondoka au ongezeko la kodi, au ardhi kutakiwa na serikali au kuvamiwa. Mashaka haya hushuhudiwa na kuchukuliwa watoto. Kama mama mmoja alivyosema, "*Mtoto wangu hushika yote haya katika akili yake wakati akiwa shuleni, bila kujua wakati atakaporudi nyumbani kama familia yake itakuwa na mahali pa kulala usiku huo*". Kutafuta njia za kupunguza mashaka haya kama vile kuwa na kazi maalumu na kipato, kushiriki katika miradi midogo midogo na kumiliki eneo dogo, ni baadhi yamikakati ambayo familia hujiwekea kwa ajili ya kutatua matatizo.

Miongoni mwa wazazi waliohojiwa 50% hawakuweza kusoma na kuandika au walikuwa na ujuzi mdogo sana wa kusoma na kuandika. Wengi hawakuwahi kwenda shule ya msingi au walikwenda tu kwa muda mfupi. utafiti haukuzingatia uelewa wa hili. Hata hivyo, wazazi wachache walielezea zaidi wakisema ni kwa sababu wao walichukua majukumu yao nyumbani kusaidia familia zao.

Watu maskini sana hujali na wanavutiwa na jumuiya waliyomo. Wao wako tayari kutetea haki za wengine. *"Ninapoona watu wananyimwa haki zao, laiti ningekuwa na elimu ya kutosha kuwa kiongozi bora na kuwa na uwezo wa kuwatetea, kwa sababu ninapoangalia watu wanaonewa najisikia kuumia sana".* Mzazi mwingine akasema, *"Tuna umoja ili kuhakikisha watoto katika jamii yetu wanakwenda shule. Hatutaki watoto kuwa wazururaji na kucheza".* Siyo vitendo pekee vinavyoonesha kwamba watu wanavutiwa na jamii zao, bali utashi wa kujua kinachoendelea na nini kinachoweza kuboreshwa. Kwa mfano katika vituo vya huduma za afya watu walisema kuna haja ya *"uongozi bora"* na *"ukaguzi wa mara kwa mara".*

Kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa iliripotiwa kama njia bora ya kuhakikisha watoto wote wameandikishwa katika shule. Pia wazazi walisema ilivyokuwa muhimu kwamba shule kuwa na uongozi bora na kuweza kukaguliwa mara kwa mara na serikali. Yote hii inaonyesha kwamba watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri huvutiwa na jamii zao na kwingineko.

Wazazi wengi walisema hushirikiana na wengine katika jamii yao. Walisema japokuwa nyakati zingine maisha katika jamii zao sio mazuri na zimejaa changamoto, hawakupenda kuhama kwenda sehemu yoyote ile kwa sababu ya kuzoea mazingira ambayo wanayoishi na kufahamiana na watu wanaowazunguka. Hata hivyo, umaskini uliokithiri unaweza kujenga na kuvunja urafiki hapo kwa papo. Wakati watu wanapoona majirani zao wanateseka wanaelewa na huwa tayari kusaidia. Wanaelewa kwamba wanaweza kuwa katika hali hiyo kesho. Wakiwa na rasilimali chache wakati mwingine maneno ya ukarimu hutolewa. Maneno haya huonekana rahisi lakini ni muhimu na huikusanya jamii pamoja.

Hizi ishara ndogo huifunga jamii pamoja ni sawa katika ngazi ya familia. Na sio mara zote kile kilichosemwa, lakini kile kilichobaki bila kusemwa, kinachohakikisha upendo na ujasiri unaohitajika kwa ajili ya familia maskini sana kuwepo. Hata hivyo, wakati shinikizo la mara kwa mara kutafuta ufumbuzi linapokuwa kubwa mno, na maneno yaliyotamkwa hatimaye hujutiwa, kidogo kidogo uvumilivu huporomoka na upendo hupotea katika machafuko. Ni katika nyakati hizi ambapo familia inaweza kuvunjika na madhara yake kwa kila mtu hasa watoto hayarekebiki.

Umaskini uliokithiri na faragha ni kinyume. Vigumu sana kuwa na faragha ukiwa unaishi katika umaskini uliokithiri, kwa kutazamwa mara zote na watu kwa kila jambo unalolifanya, unachonunua, ukiwa na kikao n.k. Hii mara nyingi hutokea na hufanya watu kuelewa visivyo, na inaweza kupelekea kuleta ugomvi. Watu maskini walisema namna gani wanavyojisikia unyonge kutokana na umaskini, kwa kuzungumza moja kwa moja, (waliambiwa wakaibe ili walipe kodi ya nyumba) au kwa vitendo(watoto kupekuliwa mbele ya watoto wenzao). Kutokuwa na faragha maana yake ni kwamba maisha ya mtu yanaanikwa na kuhalalisha udhalilishaji huo.

Kuna dhana iliyojengeka kwa watu wengi, ambayo baadhi ya watu walisema kwenye utafiti, kwamba watu maskini hawathamini elimu wala hawaipi kipaumbele. Wazo hili ni mgongano mkubwa na utafiti, kwamba wazazi hujitoa sana kuhakikisha kwamba watoto wao wanakwenda shule. Moja ya mifano mwaka uliopita ambapo mara kwa mara watoto walirudishwa nyumbani au kuadhibiwa kwa sababu hawakuleta michango ya shule, ambapo wazazi watawapa moyo kwenda tena shuleni ambapo walikutana na janga hilo hilo. Wazazi wanapowarudisha watoto wao shuleni wakijua janga litakalowapata hakika wanathamini elimu.

Kama wazazi wao, watoto pia wanajua umuhimu wa elimu. Mtoto mmoja mwenye akili sana alisema,*"Elimu hunisaidia kufikia malengo yangu. Elimu ni ukombozi kwa maisha yangu, familia yangu na kwa jamii yangu".* Ilikuwa kitu cha kuvutia sana kujifunza kupitia utafiti huu ni jinsi gani watoto walikuwa na malengo, ambayo yana kwenda bega kwa bega na uthabiti katika umuhimu wa elimu. Timu ya Utafiti imegundua watoto wamekua na malengo ya kuwa walimu, madaktari, maafisa wa polisi n.k, taaluma zote zina mchango wa kujenga jamii imara yenye umoja na taifa.

Wazazi hutarajia tumaini kubwa la baadae kwa watoto tofauti na wao wenyewe. Wanajua jinsi gani wanavyopambanana kila iitwapo leo kwa ajili ya familia zao, hatimaye wanataka matarajio tofauti kwa maisha ya baadae kwa watoto wao na wajukuu. Kama mitazamo ya watoto wao iko salama basi wanaona hapo baadaye kwao ni utulivu.

Walimu na wazazi wote huelezea umuhimu wa kushirikiana na uhusiano mzuri. Pande zote mbili hufanya juhudi, wote hupenda kuboresha, wote wana hamu ya kuboresha na kushinda changamoto. Wazazi wanaoishi katika hali ya umaskini uliokithii walisema mawasiliano na shule yanakuwepo tu pale panapokuwa na matatizo. Mara chache mzazi huenda au huitwa kwenda shuleni kwa jambo nzuri. Pale uhusiano unapoanza na uzoefu hasi inakuwa ngumu kusonga mbele. Wazazi wengi wanaelezea juu ya kwenda

shule na sio tu kusikilizwa wao. *“Lazima tukae kimya”*. Pale wazazi waliposemwa tu na hawakupewa nafasi ya kusikilizwa hawakuwa na hamu tena ya kwenda shule.

Wazazi walisema muhimu ni kwamba, mwalimu angeweza kumfahamu kila mtoto binafsi. Hii inaweza kuwa na faida, ikiwemo kuwasiliana na mzazi wa mtoto, kuelewa juu ya maendeleo ya watoto shuleni na kuelewa kama kuna mahitaji ya lazima au matatizo ya afaya.

Siku hizi karibia watu wengi wana simu za mikononi, hata hivyo utafiti umeonesha kwamba hili siyo suala. Karibia mababa wengi wana simu, lakini mamama wengi hawana. Kama ilivyo kuwa simu ni kifaa muhimu cha mawasiliano katika siku za sasa, na mama kawaida ndiye mtu muhimu katika familia kuwasiliana shuleni, hii ilijitokeza kama swali muhimu juu ya njia bora kwa walimu kuwasiliana na familia masikini sana.

Afya ya familia imehusishwa kwa uzito na pato la familia na ina uzito katika elimu ya msingi. Katika zama hizi za sera ya elimu bure Tanzania, iwapo mtoto au mzazi ni mgonjwa gharama za ziada hapana budi zipatikane. Ugonjwa unapotokea katika familia watoto wengi wanaoishi katika umaskini uliokithiri hubaki nyumbani kuangalia wazazi wao au wadogo wao au pengine kuwasaidia wazazi wao kuingiza kipato. Watoto wengine hujaribu kwenda shule wakati wanaumwa na hii huathiri masomo yao. Kupata matibabu na kuelewa umuhimu wa afya ya msingi na mlo bora ni muhimu kwa maendeleo ya mtoto na upatikanaji wa elimu.

Watu wanaoshi katika umaskini uliokithili wamenukuliwa kumgeukia Mungu kwa ulinzi na huruma. Katika kipindi cha kutokuwa na matumaini, Mungu anaweza kukupa tumaini na nguvu ya kustahimili. Pale watu wanapojisikia kutokuwa na nguvu humchukulia Mungu kama shahidi ambaye atawaongoza. Inaweza katika ubinafsi au mbele ya umma, maombi yanayotolewa kwa Mungu na watu maskini ni muhimu sana.

Watoto kutoka familia za kimaskini sana wanakumbwa na majanga ya kutoka katika kila kona kwenye jamii. Hii ina weza kutoka na kuenea kwa magonjwa kutokana na kuchangia vyoo na vifaa vya kunawia, kwenye usafiri wakati wa kwenda na kurudi shuleni kukatiza barabara na mito, uvutaji bangi na wizi, n.k. Mara nyingi watoto hujitetea wenyewe kukomesha changamoto kama hizi. Ndio maana watoto wengi wanatembea pamoja na marafiki zao wanapotoka na kwenda shule, sio tu kwa urafiki na michezo, bali kwa usalama zaidi. Urafiki ni moja ya usalama ambao watoto wamejitengenezea na ni kweli ni wanategemeana kila mmoja wao.

Kifungu cha 19 cha Makubaliano ya Haki za Mtoto zilithibisha haki za kuwalinda watoto afya ya mwili na kiakili; kifungu cha 28 kimeweka mashariti katika nchi "kuhakikisha nidhamu shuleni zina simamiwa pamoja na ubinadamu makubaliano yaliyopo"; kifungu cha 37 kinaelzea kwamba hakuna mtoto atakayeingizwa kwenye kuteswa au kufanyiwa ukatili, kumuaibisha, kumdharau au adhabu. Tume ya Haki za Mtoto inasisitizia kufasiliwa kifungu kufanya mabadiliko ya sheria mabadiriko ya sheria kuzuia adhabu ya kuchapwa watoto shuleni. kuhamasisha uzuiaji wa adhabu ya kuchapwa shuleni na kuondoa miundo ya adhabu ya kuchapwa viboko kwa watoto kumeungwa mkono na UNIESCO na UNICEF (Kuelekea utulivu shuleni kuzuia adhabu ya kuchapwa. Ripoti ya dunia 2015.)

Watoto huingiwa na woga wanapoona walimu wameshika fimbo, *"hutetemeka"* na kuogopa kumkaribia mwalimu na kuuliza maswali. Kuna mtoto alisema kumuadhibu kwa fimbo hakumfanyi asiache kufanya makosa darasani, ila tu humfanya aogope. Maoni ya watoto walio hojiwa yalisisitizia na tasisi za kimataifa na serikali ya Tanzania kama ilivyo saini na kukubaliana kwenye Haki za Mtoto kuhusu adhabu shuleni.

Wakati fedha inapohusishwa katika elimu ya msingi shuleni ambayo ingekuwa huduma ya bure, huleta ubaguzi, hutengeneza fedheha hupelekea kuvunjika kwa mahusiano kati ya wadau wa elimu. Sera ya elimu bure ilioanzishwa na serikali kuhakikisha wazazi hawaulizwi michango ya fedha ni hatua katika mwelekeo sahihi. Katika nchi ambapo sera ya elimu bure imeanzishwa, ghafla na idadi kubwa kuongezeka kwa watoto kusajiliwa, ilionekana na shule nyingi zilizidiwa. Kwa mfano, katika Sierra Leone mwaka 2010 ruzuku ambayo shule hupokea hazikutosha na malipo yalichelewa, ambayo imesababisha karo kurejeshwa. Sera mpya inahitaji kufuatiliwa ili kupunguza athari na kuhakikisha kuwa haina athari katika shule za msingi, hasa kwa watoto maskini sana.

Wazazi walikuwa tayari kuonyesha changamoto nyingi zinazowakabili walimu, uhaba wa vitendea kazi na baadhi ya watoto kuwa wakaidi, *"Nilikuwa nalaumu walimu kwamba hawafundishi, wakati ni mtoto wako mwenyewe".* Wazazi pia huzingatia mishahara ya walimu ambayo iko chini, huwapunguzia motisha, ambayo inaleta athari katika ubora wa elimu.

Ni muhimu kwamba kwa wazazi na walimu hukubaliana kuwa kuna upungufu katika mfumo wa elimu na kipi ni chanzo kikuu. Kuna umuhimu wa kutambua changamoto na kujadili nao, ingawa inaweza kuwa sio sehemu ya kuanzia. Kwa mtazamo chanya kwa njia ya ukungu wa kuchanganyikiwa unaosababishwa na matokeo yanayoweza kuchukua muda zaidi lakini unaweza kuwa na thamani kubwa kama lengo la pamoja ni makubaliano juu ya hilo.

Walimu wamejitolea kuiboresha elimu ingawa wanakutana na changamoto nyingi. Wanajitahidi kufika shule kwa wakati, kuaanda masomo, kuwakaribisha watoto kwa ukarimu, wabunifu katika ufundishaji japo kuna uhaba wa vitendea kazi na huendelea kujitoa na kuwasaidia watoto maskini. Wazazi wanasaidia juhudi hizi kwa kuwahamasisha watoto wao kujifunza, kuwapatia usalama na utulivu kutokana hali ngumu, kushirikiana na walimu na kuwa na matumaini na watoto wao kwamba wanaweza kufanikiwa. Juhudi hizi kutoka pande zote mbili ni msingi ambao hiumarisha mazungumzo kati ya wazazi na walimu.




**Timu ya Utafiti:**

**1/ Agnes Theodori Vaganjavyetu:** mtafiti, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne, mgonga mawe Tegeta

**2/ Aloyce Benjamin Chija:** mtafiti, mwalimu mkuu shule ya msingi Pwani

**3/ Feliciana Laswai:** rafiki wa ATD Dunia ya Nne, mwalimu kutoka shule ya misheni

**4/ Hamisi Mpana:** mtafiti, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne

**5/ Ibrahim Mdachi:** mtafiti, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne

**6/ Martin Kalisa:** mshauri wa utafiti huu, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne anaishi Dakar, Senegali

**7/ Mbaraka Kilima:** mtafiti, katibu mkuu wa Soko la Samaki mwanachama wa ATD Dunia ya Nne

**8/ Reachel Kayeye:** mtafiti, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne, Dar es Salaam

**9/ Rehema Abdallah:** mtafiti, mama wa nyumbani kutoka Tandale, ATD Dunia ya Nne

**10/ Robert Jordan:** mtafiti, kutoka UK sasa anaishi Mwananyamala, ATD Dunia ya Nne

**11/ Rose Ubwe:** mjumbe wa nyumba kumi, mtafiti, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne, anaishi Tandale

**12/ Salma Mosha:** mtafiti, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne, anaishi Mwananyamala

**13/ Selemani Yasini:** mtafiti, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne

**14/ Shabani Selamani Digaga:** Tegeta, mtafiti, na mgonga mawe, ATD Dunia ya Nne

**15/ Leo Beranger:** mtafiti, kutoka Ufaransa, wanachama wa timu ATD Dunia ya Nne mpaka Juni 2015

# Yaliomo


1. Muhtasari wa Utafiti........ 2

2. Utangulizi........ 4

3. Mbinu za Utafiii........ 6

4. Matokeo ya Utafiti: Changamoto gani? Ni jitihada gani?........ 12
  4.1. Binafsi........ 14
  4.2. Familia na marafiki
    4.2.1. Kupambana na matatizo........ 15
    4.2.2. Kuweka juhudi na kutafuta ufumbuzi........ 16
    4.2.3. Shughuli za ziada........ 17
    4.2.4. Matarajio ya baadaye........ 18
  4.3. Makazi na Jamii
    4.3.1. Makazi........ 19
    4.3.2. Jamii........ 21
    4.3.3. Changamoto na hofu ya jamii........ 22
    4.3.4. Nafasi katika jamii........ 22
    4.3.5. Usiri na wivu........ 23
    4.3.6. Mazingira........ 23
    4.3.7. Kuishi mahali pengine........ 27
  4.4. Kazi na kipato........ 28
  4.5. Afya
    4.5.1. Kuwa na Afya........ 30
    4.5.2. Kuumwa kwa watoto mashuleni........ 31
    4.5.3. Ambapo wazazi wanaumwa........ 32
    4.5.4. Gharama za matibabu........ 32
    4.5.5. Maombi........ 33
    4.5.6. Kwenda hospitali........ 33
  4.6. Shule
    4.6.1. Juhudi za wazazi, watoto na walimu........ 35
    4.6.2. Ushirikiano........ 38
    4.6.3. Watoto wenye ulemavu........ 42
    4.6.4. Masomo ya ziada........ 43
    4.6.5. Uji........ 45
    4.6.6. Kila kitu kuhusu elimu ni fedha........ 46
    4.6.7. Kushuka kwa elimu........ 48
    4.6.8. Urafiki........ 51
    4.6.9. Usalama/Adhabu........ 52

5. Mapendekezo........ 54

6. Hitimisho........ 56

**Picha:**
François Phliponeau, Timu ATD Dunia Ya Nne Tanzania

**Kubuni na Printing:**
Jalada by Mugisha
Mpangilio by Laurent Ganau
Printed by

**Shukrani kwa waliotafsiri na waliohakiki:**
Beth Partridge, Consepta Mahengo, Consalva Mahengo, Emma Mahengo, Saasita Munema, Salehe Seif

**Huu ni uafiti shirikishi mradi huu uliwezeshwa kwa kungwa mkona wa ukarimu na UNESCO na shirika la Maendeleo ya Ufaransa.**

**Kwa maelezo zaidi kuhusu ATD Dunia Ya Nne:**

ATD Fourth World – International headquarters
12, rue Pasteur
95480 Pierrelaye, France
(33) 1 30 36 22 11

ATD Dunia Ya Nne Tanzania
Mwananyamala. Igusule Street
P.O. Box 61786 Dar es Salaam
mailto:atd.tanzania@gmail.com

**Websites:**
International Movement ATD Fourth World: http://www.atd-fourthworld.org/
Overcoming Extreme Poverty: http://www.overcomingpoverty.org/
ATD Tanzania English: http://atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/
ATD Tanzania Swahili: http://atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/

Joseph Wresinski, mwanzilishi wa ATD Dunia Ya Nne Tanzania:
English: http://www.joseph-wresinski.org/Father-Joseph-Wresinski.html
Swahili: http://www.joseph-wresinski.org/Unaye-mama-wewe.html





**For further information:**
**ATD Fourth World**
**Mwananyamala, Igusule Street**
**P.O. Box 61786 Dar es Salaam**
**Email: atd.tanzania@gmail.com**
**Website: www.atd-fourthworld.org**

**This participatory research project was sponsored by UNESCO and Agence Français de Devéloppment**

ATD FOURTH WORLD

AGENCE FRANÇAISE DE DÉVELOPPEMENT

UNESCO